
SUPA JACKPOT
TZS. 1,144,172,464
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**JWTZ** yamsaka mpotoshaji taarifa nyongeza mshahara

UKURASA 3




UKURASA 9

# Nipashe Jumapili

Jumapili Agosti 20, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581408

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Mama auawa mtoto wake akishuhudia mita chache

UKURASA 2

# Samia: Asiyeweza kuongoza apishe

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (katikati) na Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Dk. Edwin Mhede, cheti cha mlipa gawio kubwa serikalini, wakati wa kikao kazi cha wenyeviti na watendaji wakuu wa taasisi za umma jijini Arusha jana. Benki hiyo ambayo serikali ina miliki asilimia 31.5 ilitoa gawio la Sh. biliioni 45.5 kwa mwaka wa fedha wa 2021/22. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Wadau wataka upimaji utendaji kazi mabalozi kila miezi mitatu

UKURASA 3

UKURASA WA 4

## MKANDARASI UWANJA WA NDEGE MSALATO APEWA KIBANO

SERIKALI imetoa wiki moja kwa mkandarasi SINOHYDRO CORPORATION LTD anayejenga Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Msalato, kutayarisha mkakati utakaowezesha kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hicho kabla ya Desemba, mwakani...

UKURASA WA 3

## JELA MIAKA MITANO KWA KUMCHOMA MOTO MWANAWE KISA MBOGA



MAHAKAMA ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza imemhukumu Maneno Thomas (35) mkazi wa Chamagati, Sengerema miaka mitano jela kwa kosa la kumchoma na kumwunguza mikono kwa maji ya moto mtoto wake akimtuhumu kudokoa mboga za majani...

MICHEZO YANGA KUANZA KUSAKA REKODI MPYA AFRIKA LEO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albart Chalamila, akibonyeza kitufe kuzindua rasmi mfumo wa dhamana wa bidhaa wa Kampuni ya Alaf uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Mishish Mistry Mkurugenzi Mtendaji wa Safal Group, Anders Lindgren na kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo na Meya wa jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia ataka asiyeweza kuongoza apishe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu, ameyaagiza mashirika ya umma na taasisi kubadilika katika utendaji kazi na kufanya kazi kwa ufanisi huku akisisitiza kuwa asiyeweza ni heri apishe wengine.

Pia ametaka mashirika ya umma kuacha kujiendesha kwa hasara na kuwa mzigo serikalini huku akiagiza wizara kuyasimamia na kuzionya kuhusu tabia ya kuyaingilia, kwa kutaka kupewa fedha.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akifungua kikao kazi cha wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu wa taasisi za umma, Rais Samia alisema kikao hicho kina lengo la kuboresha utendaji kazi ili kujiendesha kwa ufanisi. Kaulimbiu ya kikao hicho ni "Mageuzi Yenye Tija Kwenye Taasisi za Umma kwa Maendeleo ya Taifa."

Alisema kikao hicho cha siku tatu kitatoa dira na mwelekeo wa mashirika ya umma na utendaji wake kuboreshwa kwa muhstakabali wa taifa kiuchumi.

Rais Samia alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. trilioni 73 katika mashirika ya umma na wakala za serikali 248, ambayo baadhi yanafanya biashara na kutoa huduma kwa wananchi.

"Huu ni uwekezaji mkubwa ambao tunapaswa kujivunia. Lakini kuna maswali ya kujiuliza kuhusu tija inayopatikana katika uwekezaji huu ambapo kwa sasa mchango wa taasisi na mashirika haya katika bajeti ya serikali hauridhishi na ni chini ya wastani wa asilimia nne," alisema.

Alisema Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alipoanzisha mashirika hayo, alitaka yamilikiwe na wananchi kupitia hisa ili kuyaita mashirika ya umma, lakini umma wa Watanzania hawakuwa na uwezo wa kuzinunua.

"Siku hizi badala ya kuwa mashirika ya umma, tumekuwa mashirika ya serikali kwa sababu mengi yanategemea kujiendesha kwa fedha toka serikalini ndiyo maana nilisema sasa tubadilike. Kuna kipindi mashirika yalianza kununua hisa kwa wananchi lakini baadhi yalipotea nazo. Sasa ni wakati wa kujitafakari, wanaoweza kununua hisa na kuuza wafanye hivyo ili wawe na umiliki," alisisitiza.

Rais alisema uzoefu wa nchi zingine, mashirika na taasisi za umma, huwa na mchango mkubwa katika kuchangia maendeleo huku akitaja baadhi ya mataifa hayo kuwa ni Singapore, China, Quwait na Ethiopia.

"Hapa kwetu ni tofauti. Taasisi na mashirika yamekuwa mzigo yanakula serikalini hayarudishi kitu serikalini, hivyo yamekuwa mashirika manyonyaji. Kuna mengi yaliyosababisha mashirika yawe na mfumo huu. Nategemea hapa mtachambua na kutafuta ufumbuzi,"alisema.

Alisema kwa mfumo, mashirika yalitakiwa yawe yanajitegemea lakini hadi sasa yanachukua mshahara serikalini na fedha za kujiendeshea zinapotoka zinapangiwa kazi zingine hasa matumizi yasiyo ya lazima.

Rais alisema mashirika mengine kama ya maliasili na utalii yanafanya vizuri lakini kodi zake zinakwenda kwenye vikao nje ya nchi.

"Wizara zetu zimekuwa za kuchukua fedha kwenye mashirika haya kuleta serikalini na kuchangia hii, mara kile. Hali hii ni kinyume cha uanzishwaji wa mashirika haya. Yalitakiwa kuchangia gawio serikalini. Sasa tubadilike tuyaache yaendeshwe kimashirika na kama tunataka yaendelee tusiyaingilie," alionya.

Rais Samia alisema akiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Zanzibar alikwenda nje ya nchi kwenye maonyesho lakini hakuwa na fedha nyingine zaidi ya posho yake aliyopatiwa.

Alisema alipokutana na waziri mwenzake wa Muungano, alikusanya fedha Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Ngorongoro na huko kazi ilikuwa kuzurura kutafuta vitu vya kununua.

"Sasa nikajiuliza hii ndiyo kazi iliyotupeleka huko, sitaki hili liendelee kufanyika tukajipange katika hili, tuache kutumia fedha kinyume na makusudio, tusiweke mikono yetu huko kwenye mashirika tunayotegemea yatupatie gawio kubwa?"alihoji.

Katika hatua nyingine, Rais Samia alipongeza Benki ya CRDB kwa kufungua matawi nje ya nchi na kutaka mashirika mengine kuiga mfano huo ili yarudishe fedha nyumbani na kukuza uchumi.

**MABADILIKO MSAJILI**

Rais alisema kutokana na changamoto wanazopitia, serikali iko katika mchakato wa kutunga sheria itakayobadilisha hadhi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa mamlaka ya uwekezaji wa umma na pia uwezekano wa kuanzisha mfuko wa uwekezaji wa umma, ili kuondoa utegemezi kutoka serikalini.

Aliwasihi watendaji wake, kubadilika ili kufukuzana na sekta binafsi inayowabeba na kufanya vizuri ili uchumi wa nchi ukue zaidi ya sasa.

Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema utafiti unaonyesha duniani kuwa taasisi za umma zina mchango mkubwa wa uendeshaji wa shughuli za serikali.

Alisema katika taarifa ya Benki ya Dunia (WB) zimeonyesha kuwa zimekuwa na mali pamoja na Dola za Kimarekni trilioni 45 kwa mwaka 2015, sawa na nusu ya pato la dunia.

"Mashirika ya serikali na yasiyo ya serikali yana mchango mkubwa kwani taasisi za umma zinachangia asilimia 17 ya ajira zote katika utumishi wa umma,"alisema.

Alisema mageuzi anayofanya Rais Samia yanalenga kuongeza tija na ufanisi katika taasisi hizo, ili ziongeze utoaji huduma bora kwa wananchi.

Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, alisema ofisi yake inasimamia taasisi 248 ambazo umiliki wake ni zaidi ya asilimia 51 na taasisi 56 umiliki wake ni chini ya asilimia 51.

Alisema taasisi hizo zitaendelea kuwa chini ya Msajili wa Hazina katika utendaji wa kazi na wao wanajisimamia katika sera.

# Mama auawa mtoto wake akishuhudia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

FELISTER Danda, anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 20 na 23, mkazi wa Mtaa wa Kambarage mjini hapa, amekutwa ameuawa katika msitu wa TANWAT huku mtoto wake wa miaka miwili, Ivan Mbise akishuhudia mita chache.

Mwili wa mwanadada huyo ulikutwa huku nguo zake zikiwa zimeloa damu.

Mtoto huyo amekutwa umbali wa mita 500 kutoka kwenye tukio hilo lililotokea juzi majira ya saa tatu asubuhi katika msitu huo wa kupandwa ulioko Kata ya Ramadhani.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo huku akikemea vitendo vya ukatili vya namna hiyo.

Kasongwa aliwahakikishia wananchi kuwa wahusika wa tukio hilo watapatikana ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

"Kwa kweli tukio hili limetokea ambapo pembeni alikuwapo mtoto mdogo, imetambulika na ndugu ni mtoto wa yule dada. Matukio yanayotokea yanasikitisha kwa sababu yule mtoto mdogo pia, alikutwa ana damu, ameyashuhudia yaliyotokea atakuwa katika hali gani?

"Hatujui amekaa muda gani kule porini? Kwa hiyo niendelee kukemea vitendo viovu ambavyo vinatokea na tutahakikisha tunachunguza na kujua kiini cha mauaji haya,"alisema Kasongwa.

Nipashe ilifika nyumbani kwa Lusimiko Mwenga katika eneo la Igeleke, Mtaa wa Kambarage alikokuwa anaishi Danda, ambaye alisema amefika katika chumba cha kuhifadhi maiti katika hospitali ya Kibena na kuutambua mwili wa shemeji yake.

"Felister (Danda) ni shemeji yangu. Nilikuwa ninakaa naye hapa Igeleke kwa muda ambao alikuwa anatafuta maisha baadaye akaenda kuolewa na baada ya muda kidogo alihitilafiana na mwenzake na kwenda kutafuta maisha akapanga chumba huku tukionana na kupigiana simu tukiendelea na maisha.

"Jana watu ambao wanakaa mtaa mmoja naye wakaja kuniambia (kuhusu tukio) nikaenda dukani kwangu nikaangalia picha zinazotembea mtandaoni nikaona ni mtoto wa shemeji yangu," alisema Mwenga.

Baadhi ya majirani, akiwamo Anna Ng'ande, walisema wanamfahamu vizuri Danda na enzi za uhai wake hakuwa na matatizo na mtu.

Henry Kibiki ambaye ni Balozi wa Nyumba Kumi alisema kuwa kinachoendelea hivi sasa ni taratibu za kifamilia na mwili huo unatarajia kuzikwa katika kijiji cha Lwangu.

Diwani wa Ramadhani, Nickson Nganyange, alisema baada ya kupata taarifa hizo walifika eneo la tukio na kukuta mwili huo na baadaye walipigiwa simu na wasamaria wema kwamba, kuna mtoto kaonekana eneo la jirani ilipokuwa maiti hiyo.

## HABARI KITAIFA



Mwendesha pikipiki akiwa amepakia viroba vya mkaa katika kijiji cha Bupu wilayani Mkuranga mkoani Pwani akienda kutafuta wateja japokuwa serikali imepiga marufuku ukataji wa miti na kuchoma mkaa bila kibali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wadau wataka upimaji utendaji kazi mabalozi kila miezi mitatu

**Na Beatrice Shayo**

WANAHARAKATI na wasomi wameshauri mabalozi wanaowakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani, wawe wanatoa ripoti ya utendaji wao wa kazi kila baada ya miezi mitatu.

Wamesema lengo ni wale wasiowajibika wachukuliwe hatua mapema kabla ya Rais kupatiwa malalamiko dhidi yao.

Jumatano, Rais Samia Suluhu Hassan alifichua kasoro za baadhi ya mabalozi huku akifunguka namna mmoja wa mabalozi ambaye vitendo vyake vilisababisha mkuu wa nchi ndani ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) (bila kuitaja) kuomba mwakilishi huyo aondolewe nchini mwake.

Rais Samia alisema mkuu huyo wa nchi alimweleza namna mwakilishi huyo haonekani kazini, hashiriki mikutano na kwamba hawamwelewi.

Katika mahojiano maalum na mwandishi wa habari hii juzi kuhusiana na kasoro hizo na mapendekezo yao ya nini kifanyike, wadau hao walisema ni lazima wateule wawe wanaijua diplomasia na kuwajibika kwa maslahi ya nchi.

Mwanaharakati Bubelwa Kaiza alisema jukumu la kuhakikisha mabalozi wanafanya kazi ni la mwajiri ambaye ni serikali.

"Yaani usimamizi wa kazi zao, monitoring and evalution (tathmini na ufuatiliaji) wanachokifanya huenda una mapungufu pengine wanapelekwa huko bila kuwa na majukumu mahususi ya kufanya.

"Inategemea anavyoona aliyepelekwa huko kama alikuwa na majukumu ya kufanya wangekuwa wanadaiwa huku nyumbani, taarifa ipo wapi? Wamefikia wapi? Kwa nini haijafanyika? Ninadhani huwa hawaripoti.

"Mpaka Rais wa nchi nyingine anaishauri serikali ifanye marekebisho ina maana huku nyumbani hakuna usimamizi, tunachotakiwa ni kuongeza usimamizi na ufuatiliaji,"alisema.

Kaiza alisema jambo la kuzingatia wanaopelekwa wawe wanajua masuala ya kidiplomasia na maeneo ambayo Tanzania imejikita mfano uchumi, kijeshi, biashara, na apewe majukumu mahususi na kuwapo na utaratibu wa kutoa taarifa.

"Kama mtu haripoti taarifa zake za utendaji kazi haina haja ya kuendelea kushikilia ubalozi, anatakiwa kuondolewa hakuna sababu ya kuendelea. Anashindwa majukumu yake mpaka tunakumbushwa na nchi aliyokwenda ndiyo tunaambiwa tumuwajibishe mtu fulani, ninadhani hii si sahihi.

"Pengine tunaonekana tuna makosa kuwapeleka nje bila kujua mipango yao ya kile wanachokwenda kukifanya,"alisema.

Alisema njia mojawapo ya kurekebisha ni kuhakikisha anayepelekwa ubalozini ana maslahi mahususi yanayohitajika na kupatiwa utaratibu wa kazi ambao anatakiwa kuripoti kila baada ya miezi mitatu.

Endapo balozi hatatoa taarifa kila baada ya miezi mitatu , alisema huyo hafai na ni suala la kumrudisha mapema kabla ya Rais kupewa taarifa na mkuu wa nchi husika.

Mhadhiri Mwandamizi wa Sayansi ya Siasa na Utawala wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Richard Mbunda, alisema kauli ya Rais Samia inawaandaa kisaikolojia kwamba hajaridhishwa na utendaji wao wa kazi kwa sababu nafasi hizo ni za kuwakilisha Rais katika nchi nyingine na hupewa majukumu maalum.

"Kwa mfano ukienda sehemu ambazo ni nchi zilizoendelea ina maana unakwenda kutimiza mambo ya uwekezaji, kuvutia wawekezaji waje nchini ama watalii kwa sababu tuna vivutio vingi vya kitalii Tanzania.

"Kama ni nchi za Ulaya, Amerika ya Kaskazini unatamani uvutie watalii wengi waje nchini. Majukumu ya balozi wa nchi zilizoendelea ni makubwa, ninadhani kati ya watu walioteuliwa katika hizo nafasi kuna watu ambao hawafanyi vizuri, ni kama amewaandaa kisaikolojia huku akiwaagiza hawa wengine aliowaapisha kuwa matarajio yake ni yapi," alisema.

Mbunda alisema ni muhimu wanaoteuliwa waweze kumsaidia Rais Samia kutekeleza majukumu yao na endapo hawafanyi hivyo uamuzi wa haraka uchukuliwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini nchini (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema watumishi wa umma wote wakiwamo mabalozi wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa miongozo ya waajiri inavyowataka.

"Ninaamini wizara ina mwongozo na taratibu, mtu unapoteuliwa ama kushika wadhifa wowote iwe ni balozi au la anapewa majukumu, wanapokubali na kula kiapo wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa kiapo walichoapa,"alisema Dk. Mmari.

Alisema mtumishi wa umma ama balozi anaposhindwa kutekeleza majukumu yake ni suala ambalo halitakiwi, kimsingi kila mmoja anapaswa kuyatekeleza ili kutoruhusu kuwapo kwa malalamiko.

## Jela miaka mitano kwa kumchoma moto mwanawe kisa mboga

**Na Vitus Audax,** SENGEREMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza imemhukumu Maneno Thomas (35) mkazi wa Chamagati, Sengerema miaka mitano jela kwa kosa la kumchoma na kumwunguza mikono kwa maji ya moto mtoto wake akimtuhumu kudokoa mboga za majani.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Evod Kisoka.

Hakimu Kisoka katika hukumu hiyo alisema mahakama imejiridhisha na ushahidi katika shauri hilo bila shaka na kumkuta mshtakiwa na hatia ya kufanya ukatili dhidi ya mtoto wake.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Morice Mtoi, alidai kuwa Julai 30, mwaka huu, Thomas alitekeleza ukatili huo wa kummwagia maji ya moto mikononi mtoto huyo (jina linahifadhiwa) mwenye umri wa miaka minane, katika kijiji cha Chamagati wilayani Sengerema mkoani hapa.

Baada ya kutekeleza ukatili huo mshtakiwa, alidai kuwa alimfungia katika chumba alichokuwa akikitumia mtoto huyo ili majirani wasifahamu kilichokuwa kikiendelea.

Alidai kuwa hali ya kutokuonekana kwa mtoto huyo ilisababisha majirani kumtafuta kisha kugundua kuwa amefungiwa ndani baada ya kufanyiwa ukatili ndipo walipoamua kumkamata mtuhumiwa huyo bila kumjeruhi na kuchukuliwa na polisi.

Mtoi alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha sheria namba 169 (a) kifungu kidogo namba (1) na (2) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 Toleo la Mwaka 2022.

Mshitakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea kuhusu shtaka linalomkabili, mbali na kukiri, pia aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa mtoto wake alikuwa kero hata kwa majirani kutokana na vitendo vyake vya udokozi.

Alidai kuwa kufanya hivyo kulitokana na mtoto huyo kuendekeza tabia za utundu na udokozi kwa muda mrefu, hivyo kutaka iwe fundisho kwake na kuacha tabia za udokozi nyumbani hata kwa majirani.

Hata hivyo, mahakama ilitupilia mbali ombi hilo na kumhukumu kifungo hicho ili iwe funzo kwa watu wengine wenye tabia za kutenda ukatili dhidi ya watoto.

## JWTZ yamsaka mpotoshaji taarifa nyongeza mshahara

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limesema linachunguza kwa kina aliyehusika na upotoshaji kwamba wanajeshi wa ngazi za juu wameongezewa mshahara.

Kwa mujibu wa taarifa ya jeshi hilo, iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano Makao Makuu JWTZ, Luteni Kanali Gaudence Ilonda, taarifa hizo ni za uzushi.

"JWTZ linatoa taarifa kuwa, habari ya uzushi iliyosambazwa na mtandao wa kijamii (inautaja) kwamba wanajeshi wa ngazi za juu wa JWTZ wameongezewa mshahara ni za uzushi.

"Taarifa hiyo imeeleza kuwa ongezeko hilo limelipwa Agosti 18, mwaka huu. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaujulisha umma kuwa, taarifa hiyo ni ya uzushi na upotoshaji kwa jamii," alisema Kanali Ilonda.

Alisema ukweli ni kwamba hadi jana tarehe ya kulipwa mshahara haijafika na kwamba, hakuna ongezeko lolote au malipo yoyote kwa wanajeshi wa ngazi yoyote wa JWTZ yaliyofanyika tarehe iliyotajwa na mtandao huo wa kijamii.

"JWTZ linaendelea kufuatilia na kuchunguza kwa kina aliyehusika na upotoshaji huo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA MOROGORO MJINI
KITUO CHA MJINI, MKOA WA MOROGORO

Usimamizi wa Mirathi Na......88/2023

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: LEONARD HENRY KAZIMOTO wa MAFISA

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA SAIDI JAKSON

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 15Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2023

..............................................
HAKIMU

# Ofisi DC yalia kuzidiwa kesi migogoro ya ardhi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WILAYA ya Kahama mkoani Shinyanga, imeeleza kukabiliwa na migogoro mingi ya ardhi ambayo imekuwa ikiripotiwa katika ofisi hiyo huku Jumuiya ya Maridhiano na Amani ikipewa jukumu la kuishughulikia inayohitaji maridhiano.

Ofisa Tarafa ya Kahama Mjini, Julius Chagama, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, aliyasema hayo juzi wakati wa hafla ya kusimika viongozi wapya wa jumuiya hiyo.

Alisema kuwa kwa sasa ofisi hiyo imeelemewa na migogoro hiyo na kuomba ushirikiano wa kuitatua.

"Kila siku ya Jumatatu hadi Ijumaa, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imekuwa ikishughulikia migogoro ya ardhi kwa wingi kulinganisha na migogoro mingine inayoripotiwa ikiwamo ndoa, ugomvi na madeni," alisema.

Chagama alisema mara nyingi migogoro hiyo inakuwa ya kifamilia, ukoo kwa ukoo ambayo inaweza kuisha kwa maridhiano kwa kukalishwa chini na kushauriwa nini cha kufanya na kuondoa usumbufu wa kuifikisha katika Baraza la Ardhi.

"Na hili ombi nimetumwa na mkuu wetu wa wilaya niwafikishieni hapa ili tumalize migogoro hii huko kwenye ngazi za chini na kuepuka gharama zisizo za lazima,"alisema Chagama.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Shekhe Amir Hassani, alikiri kuwapo kwa migogoro hiyo na kuahidi kuitatua kwa kushirikiana na viongozi wenzake na ile ambayo wataishindwa wataifikisha katika vyombo vya sheria.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuitangaza jumuiya hiyo katika ngazi za Halmashauri za Msalala na Ushetu kwa kutafuta viongozi wawakilishi kutoka madhehebu ya dini ya Kiislam na Kikristo ili zile zinazohitaji kutatuliwa huko zitatuliwe.

Shekhe Hassani aliomba wapatiwe ofisi karibu na Mkuu wa Wilaya ili iwe rahisi kuwapata wateja hao wanaofika mara kwa mara.

Makamu Mwenyekiti wa jumuiya hiyo Mkoa wa Shinyanga, Askofu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Emmanuel Makala, alisema, "Mahakama zetu zimelemewa na kesi nyingi ambazo baadhi zinahitaji kusuluhishwa kwa njia ya maridhiano.

"Tukuahidi kuzitumia ofisi zetu katika kuzisaidia Ofisi za Wakuu wa Wilaya pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika kushughulikia migogoro mbalimbali inayogusa jamii moja kwa moja," aliahidi.

# Mkandarasi uwanja wa ndege Msalato apewa kibano

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetoa wiki moja kwa mkandarasi SINOHYDRO CORPORATION LTD anayejenga Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Msalato, kutayarisha mkakati utakaowezesha kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hicho kabla ya Desemba, mwakani.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Balozi Aisha Amour, alitoa maagizo hayo jana pia kwa Mshauri Mwelekezi M/S BEZA na Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Dodoma.

Balozi Amour alitoa maagizo hayo baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kiwanja hicho na kutoridhishwa na kasi ya ujenzi inavyokwenda.

"Kwa kweli sijaridhishwa na kasi yenu, ninataka mnipe mkakati utakaowezesha kiwanja hiki kukamilika kwa wakati na kwa viwango," alisema.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Msalato awamu ya kwanza unahusisha barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara za maungio, maegesho ya ndege na uzio wa usalama.

Pia unahusisha barabara ya kuingia na kutoka kiwanja cha ndege, maegesho ya magari na usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege.

Hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 30.91, wakati awamu ya pili ya ujenzi huo ukihusisha ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake.

Balozi Amour pia alikagua ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje wa Dodoma (Dodoma Outer ring road) ambayo ina sehemu mbili, Nala- Veyula- Mtumba -Ihumwa Dry Port kilometa 52.3 na sehemu ya pili Ihumwa -Matumbulu -Nala kilometa 60 na kuwataka makandarasi wa miradi hiyo nao kuja na mikakati itakayowezesha kwenda kwa kasi kabla ya mvua za Elnino kuanza.

"Tusingependa visingizio vya mvua kwa sababu Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imeshatuonya kutakuwa na mvua nyingi, ni vizuri kazi zinazotakiwa kufanyika sasa zikafanyika mapema ili kuepuka usumbufu," alisema.

Mkandarasi wa China Civil Construction Corporation anayejenga sehemu ya kwanza na ya pili ameahidi kutekeleza maelekezo hayo ili kukamilisha ujenzi huo kwa mujibu wa mkataba na katika ubora stahiki.



Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, (Sekta ya Ujenzi), Balozi Aisha Amour, akitoa maelekezo kwa Mshauri mwelekezi wa Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, Mhandisi Shegan Berharie, alipokuwa akikagua maendeleo ya mradi huo jana, mkoani Dodoma. **PICHA: WJU**

# Parole yagomea maombi kuachiwa wafungwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Taifa ya Parole imesema haijaridhishwa na mapendekezo ya kuwaachia huru wafungwa 16 walioomba kuachiwa huru kupitia sheria ya msamaha kwa wafungwa.

Wafungwa hao ni waliokutwa na makosa ya ujangili na mauaji.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapa katika kikao cha 48 cha Bodi hiyo, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Balozi Khamis Kagasheki, alisema wafungwa hao wameshindwa kukidhi vigezo kutokana na kukutwa na makosa hayo na kuharibu rasilimali za utalii wa nchi.

"Bodi haijaridhia maombi ya wafungwa 16 kuachiwa huru na hii imetokana na kukutwa na makosa ambayo hawapaswi kuachiwa huru," alisema Balozi Kagasheki.

Aidha, alisema bodi hiyo inawasilisha majina 12 ya wafungwa waliokidhi vigezo vya kuachiwa huru kupitia sheria hiyo kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuridhia maamuzi hayo.

Balozi Kagasheki aliwataka wafungwa watakaoachiwa huru kubadilika kitabia na kuwa raia wema.

"Jeshi la Magereza linaendelea kuweka utaratibu wa kutoa elimu kuhusiana na sheria ya Parole kwa jamii ili kuitofautisha na ile ya msamaha wa Rais ambapo nao kuna baadhi ya wafungwa huwa wanaachiwa huru," alisema.

"Jamii iwapokee watu hawa ambao wataachiwa huru kwa sababu mpaka kupitishwa bodi hiyo imepita sehemu mbalimbali, ikiwemo kuuliza ndugu, waathirika wa makosa waliotendewa na watu hao kama wapo hai pamoja na kamati za wilaya,mkoa hadi taifa," alisisitiza.

Kaimu Kamishna wa Sheria na uendeshaji wa Magereza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Boyd Mwambingu, alisema kuna mambo ambayo wameangalia katika wafungwa hao walioomba kupatiwa msamaha.

Mwambingu aliishukuru Bodi ya Parole kwa kutoa maamuzi kwa kuangalia maslahi mapana ya nchi.

Awali, Kamishna Jenerali wa Magereza, Ramadhan Nyamka, alisema bodi hiyo itaendesha kikao hicho kwa kuzingatia sheria hiyo na kusisitiza haki itatendeka katika utoaji maamuzi hayo.

HABARI KITAIFA

# Kariakoo wamsifu Rais Samia kuondoa kero

**Na Mary Geofrey**

WAFANYABISHARA wa Soko la Kariakoo, Dar es Salaam, wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusikiliza na kuondoa kero zilizokuwa zinawakabili kwa muda mrefu.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi sokoni hapo, walisema kwa sasa wana uhuru wa kufanya biashara bila bugudha.

Mfanyabiashara katika soko hilo, Bernard Athanas, alipongeza serikali kwa kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero zao zilizokuwa zinawakabili kwa muda mrefu na sasa wanafanyabiashara kwa utulivu.

Kuhusu kuadimika kwa Dola, Athanas alisema kumeathiri uagizaji wa mizigo kutoka nje ya nchi na kufifisha biashara.

Alisema mizigo wanayoagiza nje wanalazimika kubadili Shilingi kuwa Dola ili kupata bidhaa.

Alisema kuadimika kwa dola kunasababisha gharama za kuagiza mizigo kutoka nje kupanda, hivyo kusababisha bidhaa kupanda bei.

"Kwa sasa Dola imeadimika, kupatikana kwake ni kitendawili lakini pia ukiagiza gharama nazo za bidhaa zinaongezeka kwa sababu ya kupanda huku, tunaiomba serikali iingilie kati kuona namna ya kutusaidia," alisema.

Barnabas Kimambo, alisema licha ya utulivu uliopo Kariakoo hivi sasa, uhaba huo wa Dola umeathiri kwa kiasi kikubwa uzungushaji wa mitaji yao na hivyo kuwa tishio kwa uchumi.

Mwenyekiti wa Wafanyabishara sokoni hapo, Martin Mbwana, alisema kwa sasa upatikanaji wa fedha hizo za kigeni umekuwa changamoto kubwa kwao na wengi wao wanazitegemea kuagiza bidhaa nje ya nchi.

"Hali hii kwa sasa inatuweka katika wakati mgumu kibiashara sokoni Kariakoo, ila shughuli zetu zinakwenda vizuri na tunafanya biashara kwenye utulivu mkubwa baada ya Rais Samia kusikiliza kero zetu kupitia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa," alisema Mbwana.

Hata hivyo, alisema kamati iliyoundwa awali kuhusu kero zao bado haijawasilisha taarifa na majibu yake hivyo, wanaendelea kusubiri huku wakiendelea kufanyabiashara kwa utulivu bila kusumbuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).




Mtambo wa Kampuni ya Ujenzi ya Sinohydro na mafundi wa kampuni hiyo wakiendelea na ujenzi wa barabara ya mabasi ya mwendokasi katika eneo la Banda la Ngozi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tanzania, Malawi bega kwa bega sekta uchukuzi

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na Malawi zimeweka nia ya kushirikiana katika usafiri kwa njia ya barabara, huduma za bandari katika Ziwa Nyasa na na uhudumiaji wa wa mizigo ya Malawi katika Bandari ya Dar es Salaam.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuizi, anayesimamia Sekta ya Uchukuzi, Gabriel Migire, alisema hayo juzi kwenya mkutano uliowakutanisha makatibu wakuu wa sekta ya uchukuzi toka Tanzania na Malawi. Lengo la mkutano huo lilikuwa uboresha usafirishaji kwa njia ya Barabara.

"Malengo mengine ni Huduma za bandari kwa Ziwa Nyasa kwa kuwa ziwa hili lipo katika pande mbili yaani Tanzania na Malawi pia kuendelea kuwashawishi kutumia bandari ya Dar es Salaam," alisema Migire.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Usafirishaji wa Umma kutoka Malawi, Hastings Chiudzu, alisema ni muhimu kwa wizara hizi kushirikiana na kuondoa changamoto mbalimbali za usafirishaji

Pia katibu mkuu huyo alisema ataendelea kuwashawishi wafanyabishara wa Malawi kuendelea kutumia bandari ya Dar es Salaam kwa kuwa ina utaratibu mzuri wa kushusha na kupakia mizigo.

Wataalam hao kutoka Malawi walitembelea ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na bandari ya Dar Es Salaam na kuipongeza serikali ya Tanzania kwa kutekeleza mradi huo Mkubwa wa reli Pamoja na upanuzi wa bandari.

# LATRA yaalika wadau maoni usafiri usiku

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), imewaalika wasafirishaji kuanza kupeleka maombi ili yachakatwe kwa ajili ya maandalizi na kujipanga kuanza kutoa huduma hiyo kwa saa 24.

Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabarani wa LATRA, Johansen Kahatano, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari. Alisema baada ya kupokea maombi hayo hatua itakayofuata ni kuyachakata, kujua ukubwa wa maeneo yenye uhitaji na kupanga ratiba za kuanza huduma hiyo kwa kupanga ratiba za njia gani zianze kulingana na ukubwa wa mahitaji.

"Tunatarajia kwamba huduma hii haitachelewa sana kuanza kwa sababu uhitaji wa kutoa huduma hiyo saa 24 upo na wizara zote mbili za Mambo ya Ndani ya Nchi, na Ujenzi na Uchukuzi kukaa pamoja.

"Kwa hiyo tunaamini kwamba mpaka tumalize kuchakata maombi ambayo tutapokea kutoka kwa wasafirishaji, Wizara hizi zitakuwa zimeshakaa pamoja. Kama ambavyo tulianza huduma ya usafirishaji saa 11 alfajiri na baadae saa tisa, ndivyo tutachakata na kupanga ratiba hivyo hivyo kwa hii ya saa 24, kwamba njia gani zianze kutokana na ukubwa wa uhitaji wake," alisema. "Kwa hiyo tunachosisitiza ni kwa wenye nia ya kutoa huduma waanze kuleta maombi hayo ili serikali ikianza kufanya uamuzi ijue uhitaji ni mkubwa kiasi gani, kwa maeneo yapi, idadi ya gari zilizoomba kutoa huduma na kama wanakidhi vigezo."

Mwishoni mwa Juni, mwaka huu, akiahirisha Bunge la Bajeti, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na ile ya Ujenzi na Uchukuzi kukaa pamoja kuona namna ya kuweka utaratibu utakaofuatwa na wasafirishaji hao ili waanze kutoa huduma hiyo kwa saa 24. Katika hatua nyingine, Kahatano alikemea baadhi ya wasafirishaji ambao wameanza kukiuka taratibu za usafirishaji kwa kutoa huduma kinyume na ratiba walizopangiwa.

"Lakini hivi karibuni tumebaini kuna baadhi ya wasafirishaji ambao wameanza kutoa huduma kinyume na ratiba zao walizopangiwa. Hili ni kosa na tutawachukulia hatua kali.

"Kila gari linalotoa huduma ya usafirishaji limepangiwa ratiba yake, zipo za saa 12 na 11 alfajiri pamoja na za saa tisa. Kila mmoja anapaswa kuzingatia ratiba yake. Kuna kampuni tatu tumezibaini zimeanza kutoa huduma hiyo kinyume na ratiba zao, lazima hatua kali zichukuliwe dhidi yao," alisema. Pia, alisema wanaendelea kufuatilia na kuwachukulia hatua madereva wanaoendesha kwa mwendokasi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Alichosema Rais kiwe funzo mabalozi katika utendaji wao

**MAPEMA** wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan aliwaapisha mabalozi wapya wanaoiwakilisha nchi katika mataifa mbalimbali katika hafla iliyofanyika Ikulu, Chamwino jijini Dodoma. Mabalozi hao waliteuliwa kuchukua nafasi za mabalozi waliokuwapo awali katika nchi hizo kustaafu, kumaliza muda wao au kuhamishwa vituo vya kazi.

Licha ya kuwaapisha, Rais Samia aliwahutubia wateule hao na kuwaelekeza juu ya wajibu wao katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Aliamua kufanya hivyo kutokana na baadhi yao kubainika kuwa wamekuwa goigoi au hawajui nini wanachopaswa kufanya katika kazi hiyo huku akibainisha kuwa miongoni mwao wanadhani ni kuhudhuria mikutano na sherehe. Hatua hiyo, alisema haileti manufaa wala kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa kwa nchi kuwa na mwakilishi katika taifa fulani.

Katika kuwaelekeza juu ya wanayopaswa kufanya katika kazi zao, Rais alisema mabalozi hao wanatakiwa kufuatilia na kusimamia utekelezaji baadhi ya makubaliano na mikataba ambayo Tanzania imeingia na nchi hizo. Sambamba na hayo, wanatakiwa kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kutangaza fursa zilizoko Tanzania na pia ushirikiano wenye manufaa kwa pande husika katika masuala ya kiuchumi na kijamii.

Bila kuuma maneno, Rais Samia alibainisha kwamba katika nchi fulani barani Afrika, kiongozi mkuu wa taifa hilo alimwambia kuwa hamtaki balozi aliyekuwa akiiwakilisha Tanzania kwa sababu ya kutotekeleza majukumu yake. Alisema balozi huyo alilalamikiwa kuwa haonekani katika shughuli zake na amekuwa mtu wa kuhudhuria sherehe na kuwapo wakati viongozi wakuu wa nchi yake wanapotembelea nchi hiyo!

Hotuba ya Rais Samia kwa mabalozi hao inaweza kuelezwa kuwa ni dawa ambayo itatibu maradhi yaliyokuwa kwa wawakilishi wa nchi ughaibuni na sasa watafanya kazi wanazopaswa kuzitenda. Ni wazi kwamba haiingii akilini mtu anateuliwa kuiwakilisha nchi lakini hakuna matunda yanayotokana na kuwapo kwake katika taifa husika. Yako mambo ya kufanya katika mataifa hayo hasa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi pamoja na kujifunza mambo mazuri yaliyoko katika nchi hizo na kuyaleta Tanzania.

Kwa sasa Tanzania mtazamo wake ni kuendeleza uchumi kupitia uwekezaji katika sekta mbalimbali. Kwa mantiki hiyo, balozi anayeiwakilisha nchi kwenye taifa husika anapaswa kutumia nafasi yake kushawishi wawekezaji katika kilimo, utalii, viwanda, sayansi na teknolojia sambamba na kutafuta nafasi za Watanzania kunufaika kibiashara na elimu.


Katika elimu kwa mfano, mabalozi wanatakiwa kuangalia fursa za masomo ya elimu ya juu katika vyuo vilivyoko katika nchi hizo ili kuwezesha vijana wa Kitanzania kusomea fani mbalimbali na hatimaye kurejea nchini kulitumikia taifa katika sekta ya umma au binafsi. Licha ya kunufaika kimasomo, vijana hao wanaweza kutumia fursa hiyo kushawishi marafiki zao kuja kuwekeza nchini katika miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Ili kufanikisha hayo, mabalozi wanapopangiwa vituo vya kazi wanapaswa kujua masuala mbalimbali yanayohusu nchi wanazokwenda kuiwakilisha Tanzania zikiwamo shughuli za maendeleo na sekta zilizosababisha zikapiga hatua kwenye nyanja mbalimbali.

Kwa mtu anayekwenda Japan, China, Korea Kusini na Malaysia, mathalan, anatakiwa kujifunza sababu zilizofanya nchi hizo kupiga hatua kimaendeleo ili ujuzi huo usaidie nchi kusonga mbele kiuchumi. Nchi hizo zimepiga hatua katika viwanda, biashara, sayansi na teknolojia, hivyo ni fursa kwa Tanzania kujifunza na kutafuta fursa pamoja na kuvutia wawekezaji kuhawilisha mambo hayo nchini.

Kwa kufanya hivyo, wanaweza kusaidia nchi kusonga mbele kiuchumi na huduma za kijamii. Licha ya kuiwezesha nchi kupata maendeleo chanya ni dhahiri kwamba wataacha alama isiyofutika katika utumishi wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ulazima masomo ya sayansi uendane na uwapo wa wataalam wa maabara

**UFAULU** wa wanafunzi katika masomo ya sayansi umekuwa ukikabiliwa na changamoto na kuibua sintofahamu kama lengo la serikali la safari ya kuelekea uchumi wa viwanda linaweza kutimia.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeamua kufanya masomo hayo kuwa ya lazima kwa wanafunzi wote wa sekondari kuanzia kidato cha kwanza.

Ni tangu mwaka 2016, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitangaza uamuzi huo, ikiwa ni kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, ambapo serikali ilibainisha kuwa inataka kuufanya uchumi utegemee viwanda.

Hivyo, mkakati huo wa uchumi kutegemea viwanda hauwezi kukamilika bila kuwa na wataalam wa fani mbalimbali waliobobea katika masomo ya sayansi, ndipo ikatangaza kuwa masomo ya sayansi sasa ni lazima.

Lengo la serikali ni zuri lakini linakutana na kikwazo njiani ambacho ni ukosefu wa wataalam wa maabara katika shule zake, hali inayoweza kusababisha wanafunzi wasisome masomo hayo kwa vitendo.

Ukosefu huo wa wataalam wa maabara katika shule mbalimbali za umma unajitokeza wakati serikali imeshatangaza mkakati huo, jambo ambalo ninadhani ipo haja ya kusambaza wataalam hao mapema.

Mfano mmojawapo wa ukosefu wa wataalam hao ni Shule ya Sekondari Abuu Jumaa iliyopo Kata ya Kivule, Dar es Salaam. Baadhi ya wanafunzi wake waliwahi kulalamikia ukosefu huo.

Kwa mujibu wa wanafunzi hao, walimu wa masomo ya sayansi ndio wanaogeuka kuwa wataalam wa maabara, kitendo ambacho wanaamini kwamba hawawezi kufundishwa kikamilifu, kwa kuwa walimu hao si wataalam.

Haiwezekani kufikia uchumi wa viwanda bila kuwa na wasomi wa sayansi kwanza, lakini pia haiwezekani kufanikiwa katika masomo hayo bila kuwa na wataalam wa maabara ambao wangesaidia kufundisha wanafunzi kwa vitendo.

Kwa kuwa nchi imeamua kuwa na wanasayansi wa ndani kuliko kutegemea kutoka nje, basi ingekuwa ni vyema kama jitihada zitafanyika ili kuhakikisha kila shule ya umma inakuwa na wataalam hao.

Awali, wanafunzi wanaosoma elimu ya sekondari walikuwa wanaweza kuchagua aina ya masomo watakayo wafikapo kidato cha tatu na kuacha mengine, lakini baadaye ikatangazwa kuwa masomo ya sayansi ni ya lazima kuanzia kidaoto cha kwanza hadi cha nne.

Mwongozo huo mpya uliotangazwa na serikali, ni vyema sasa kila shule ikiwa na wataalam wa maabara, kwani ninaamini ni njia nzuri ya kupata wasomi wengi waliobobea katika fani mbalimbali.

Kwa masomo hayo, sidhani kama kinachoangaliwa ni mwanafunzi kupata alama za juu pekee bali pia awe na uwezo wa kugundua baadhi ya vitu kupitia elimu aliyopata na kutatua changamoto katika jamii.

Uwezo wa kufanya hivyo ni hadi asome masomo ya sayansi kwa vitendo, ambavyo vinategemea uwapo wa wataalam wa maabara katika shule. Hivyo ingependeza kama nguvu kubwa itaelekezwa huko.

Ni kweli juhudi kubwa zimefanyika na kusaidia shule nyingi za umma kuwa na majengo kwa ajili ya maabara, tatizo lililobaki sasa ni ukosefu wa watalaam hao ambao wangesaidia wanafunzi kuwa na ujuzi zaidi.

Wataalam wa masomo ya sayansi, wanaweza pia kusaidia wanafunzi kuwa wabunifu wa mambo mbalimbali na hata kuweza kujiajiri au kutatua changamoto zinazowazunguka katika jamii yao.

Ninaamini matamanio ya kila mpenda elimu, ni kuona mwanafunzi anakuwa na uwezo wa kugundua kitu kitakachotatua changamoto katika jamii na ni lazima aweze kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali.

Hayo yote yanaangukia kwenye sayansi ambayo mwanafunzi amefundishwa kwa vitendo, si kwa nadharia tu kwa sababu ya ukosefu wa wataalam, hivyo uwapo wa watu hao katika shule ungepewa uzito.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Chonde Watanzania tusishabikie uhaini



Pascal Mayalla

KUTOKANA na tishio la matamshi yenye viashiria vya uhaini dhidi ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) kutoka kwa baadhi ya watu na wahusika kushikiliwa na vyombo vya dola, wameibuka watu, mashirika, wanaharakati kupigia kelele kwamba kuna kesi ya uhaini.

Hali hiyo imesababisha hata baadhi ya taasisi za kimataifa zimetaka kuingilia kati mambo yetu ya ndani. Kwa kuwa mimi mwandishi wako wa makala hii pia ni mwanasheria na wakili wa kujitegemea, naomba kuitumia safu hii ya leo kuanza mfululizo wa makala elimishi kuhusu katiba, sheria, haki na wajibu.

Naomba nianze na elimu fupi kuhusu makosa mawili makubwa kuliko yote kwenye katiba yetu. Makosa haya ni kosa la kuua (murder) na uhaini (treason). Makosa yote haya mawili adhabu yake ni kifo. Kwa Tanzania inatekelezwa kwa kunyongwa mpaka kufa. Kwa nchi yetu tuna gereza moja tu la kunyongea ambalo ni la Isanga, lililoko Dodoma.

Mtu akihukumiwa kifo, adhabu hii haitekelezwi mpaka kwanza itiwe saini na Rais wa JMT hati inayoitwa Hati ya Kifo (death warrant).

Awamu ya kwanza ya utawala wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, uliodumu kwa miaka miaka 23, zilitiwa sani hati mbili tu.

Awamu ya pili ya miaka 10, Rais Ali Hassan Mwinyi, alitia saini hati kadhaa. Awamu zilizofuata za Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete na Dk. John Magufuli, hakuna hati yoyote iliyotiwa saini ndiyo maana sisi watetezi wa haki za binadamu, tunapendekeza adhabu hii ifutwe.

Si kila mauaji yakifanyika ni kesi ya mauaji. Kuna mauaji yanaweza kufanyika na ikawa si kesi ya mauaji bali ya kuua bila kukusudia (manslaughter). Ili iwe kesi ya mauaji, lazima kufanyike mambo mawili, kwanza, ni kitu kinachoitwa kitendo cha mauaji, na pili ni nia ovu ya kutenda mauaji, yaani dhamira ya kuua au kukusudia kuua.

Uhaini umetajwa kwenye sura ya Saba kifungu cha 39 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu. Kifungu cha 39 ( 1 ) cha kanuni za adhabu kinasema mtu yeyote ambaye yumo ndani ya Jamhuri ya Muungano au popote, kujaribu kumuua Rais, kuanzisha vita dhidi ya Jamhuri ya Muungano, kusababisha, kuwezesha, kuchochea, kushawishi, kushauri kuhusu kifo, kumlemaza, kumzuia, kufungwa kwa Rais.

Kwa mujibu wa sheria tuliofundishwa darasani kuwa uhaini ni vitendo na si kauli ambayo ni uchochezi.

Kwa vile mpaka sasa hakuna mashtaka yoyote ya uhaini yaliyofunguliwa katika mahakama yoyote, nawaomba Watanzania wenzangu tusishabikie uzushi wa uhaini. Hili si jambo la heri hata kidogo.

Vivyo hivyo kwenye jinai ya uhaini, si kila matamshi ya uhaini ni uhaini. Ili kuwapo kwa jinai ya uhaini, lazima kuwapo sifa kuu mbili, ya kupanga kufanya uhaini. Kitendo cha mtu ameghafilika tu na hoja za Club House, akaanza kutoa matamshi ya kupindua serikali, haimaanishi ni uhaini wa kupindua kweli serikali. Lakini matamshi hayo yanaweza kuwa ni matamshi ya uchochezi, hivyo kusababisha watu wapange kweli kupindua serikali.

Lakini matamshi tu kama matamshi bila kuwapo kupanga kupindua serikali, watu hao watakuwa wamefanya uchochezi na si uhaini.

Kitendo cha watu hasa wanaharakati kupigia kelele uhaini, kuiogopesha dunia na kufanya nchi kuangaziwa kimataifa, wakati hadi ninapoandika hapa, hakuna kesi yoyote ya uhaini iliyofunguliwa popote, hivyo kushabikia na kushadadia uhaini ni kutaka kumchafulia Rais Samia Suluhu Hassan sifa yake kuu ya kuliponya taifa.

Tanzania toka tumepata uhuru, tumewahi kuwa na kesi tano za uhaini. Kesi ya kwanza ni ile ya maasi ya jeshi ya Januari 18, 1964 siku sita baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Jeshi ya King's African Rifles (KAR) liliasi, likavunjwa na hatimaye kuundwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Kesi hii iliendeshwa kijeshi, hivyo wala sijui matokeo yake.

Kesi ya kwanza ya uhaini katika Mahakama ya wazi ni kesi ya kina Bibi Titi Mohamed, John Lifa Chipaka, Michael Kamaliza na wengine ya mwaka 1971 baadaye ikaja kesi ya uhaini inayomhusu Juma Thomas Zangira.

Mwaka 1982 ndipo kulifanyika kesi ya uhaini ya watu 38, wakiongozwa na Pius Lugangira na Hatibu Ghandi. Kinara wa kesi hiyo ni Komandoo Martin Tamimu aliyeuawa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Hapa katikati kukatokea kesi ya mwisho ya uhaini Zanzibar ya kina Seif Sharif Hamad, Shaaban Khamis Mloo, Juma Duni Haji, Machano Khamis Ali , Hamad Rashid Mohammed na wengine 18 wa Chama cha Wananchi (CUF). Kesi hii ikatupiliwa mbali baada ya Mahakama Kuu kutamka kwamba Zanzibar si nchi, hivyo jinai ya uhaini haiwezi kutendeka.

Ili kuwasaidia Watanzania kuzijua haki zao, Jumapili ijayo nitaanza kujitolea kuelimisha umma kuhusu katiba, sheria, haki na wajibu. Somo la kwanza litakuwa kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Wasalaam**
**Paskali**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania hili lisitugawe tukaparaganyika



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WATANZANIA tumegawanyika. Sakata la Dubai Port World (DP World) limetugawa dhahiri. Watanzania tuko kambi mbili za wazi kabisa. Kuna inayounga mkono mkataba wa bandari na kuna inayopinga mkataba huo, kila upande na sababu zake.

Kambi moja inasema mkataba huu haufai kwa sababu una matatizo, lakini nyingine inasema hakuna mkataba bora kama huu utakaoliletea taifa maendeleo makubwa kiuchumi. Lakini kambi zote zinaunga mkono uwekezaji.

Hata hivyo, hilo la wote kuunga mkono uwekezaji linazibwa na kambi zinazopingana kwenye mkataba na kufanya tutazamane kama maadui ndani ya nchi moja, kisa ni Dipiiweldi kuja kukaa Tanzania na kufanya biashara.

Leo mazungumzo ya Watanzania ni mkataba mbaya, mkataba mzuri! Mbona ni tofauti na ilivyokuwa mwaka 1978 pale majeshi ya Nduli Iddi Amin yalivyovamia ardhi ya Tanzania na tukaamua kupambana nayo mpaka ushindi?

Katika kadhia ya Amini, tukiwa chini ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mbona lugha yetu ilikuwa moja? Tulikuwa tukisema kwa kujidai kwamba: Sababu tunayo! Nia tunayo na uwezo tunao! Na tulishinda.

Hakika hakuna kipindi Watanzania walishikamana kwa umoja thabiti kama ule kiasi cha kujitolea kwa hali na mali kwenda mstari wa mbele kupambana na kuyang'oa majeshi ya Uganda kwenye ardhi ya Tanzania.

Imekuwaje safari hii lugha zinagongana kila kambi na lugha yake? Tumefikishana mpaka mahakamani kuhusu mkataba na Mahakama imeamua ilivyoamua. Kambi moja ikashangilia na nyingine ikanuna.

Iliyonuna ikasema inarudi mahakamani kutafuta haki ya ziada! Lakini pia ikasema itaandaa maandamano yasiyo na ukomo nchi nzima! Miongoni mwa wasemaji wakavuka mpaka na vyombo vya usalama vikaona isiwe shida. Tuwe nao watufafanulie kauli zao.

Kwa vyovyote vile, kampuni hii itatia mguu nchini kwa jinsi mambo yanavyokwenda na jinsi mkataba ulivyo, ina maana mgawanyiko utaendelea, kwa sababu ikija wapingaji watanuna na isipokuja kambi nyingine itanuna.

Viongozi wetu wana kazi ya kutubadilisha, ili tukae pamoja na tuendelee kuijenga nchi yetu na amani yetu kwa pamoja kama Watanzania tulivyolelewa, ili kampuni la kigeni lisituweke pabaya.

Sitaki kuamini, kwamba katika mazingira haya ya sasa, kampuni hiyo bado itataka kuja kuwekeza bila kuhofia nini kitafuata, kutokana na kundi kubwa la watu wanaoonesha dhahiri kukataa kata kata kuipokea!

Hakuna jambo gumu kama kumlazimisha punda kunywa maji. Kama hataki kuyanywa ni bora akaachwa abaki na kiu yake kama anayo kweli, kwa sababu kumlazimisha anaweza kurusha teke likatudhuru.

Amani katika nchi yoyote ina gharama kubwa, ndiyo sababu kuna vyombo vinalipwa ili kuhakikisha inadumu. Kama ndivyo, na kwa kuwa inaonekana uwekezaji huu unataka kuhatarisha amani yetu, lifanyike jambo.

Watanzania tukubali kuingia gharama kwa kuandaa upigaji kura ya maoni ili tuone ni wangapi wanakubaliana na mkataba huu kama ulivyo na kama ni wengi basi wapewe huku wachache ambao ndio wanaunga mkono wasikilizwe.

Ikumbukwe kwamba katika miaka ya 1990, tulifanya utafiti ambao ulituwezesha kurejea kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini na sasa tumo humo.

Ilikubaliwa baada ya wachache kusikilizwa lakini pia muktadha ulitazamwa, kwani waliokubali kurejewa kwa mfumo wa vyama vingi walikuwa asilimia 20 dhidi ya 80 waliokataa, lakini tukarejea kwenye vyama vingi.

Sasa kama inawezekena, basi utafiti wa aina hiyo au kama si kupiga kura, ufanyike ili tujue kwa uhakika kama tunaukubali mkataba huu au hatuukubali na hivyo tufikie uamuzi wa kusuka au kunyoa.

Hivi sasa kinachoonekana ni kwamba wanasiasa wamegawanyika, wataalamu wamegawanyika, viongozi waliopo na waliostaafu wamegawanyika lakini pia wanahabari wameonesha mgawanyiko mkubwa katika hili.

Watanzania tukae chini tutafakari tuone nini cha kufanya ili tusijikwae tukaanguka na kuchekwa na wenzetu, hususan wanaotuonea wivu wakitaka tuanguke ili wao wachukue fursa.

Yawezekana tunaonewa wivu, kwamba tunaingia mkataba na DP World lakini pia yawezekana tunachekwa jino pembe, kwamba tukiingia tu tumekwisha.

Hivyo, kinachotakiwa ni tafakari ya hali ya juu na kuacha kukimbizana kuingia mkataba ambao wachache wanaamini uko sawa, huku wengi wakiona hauko sawa. Nchi hii ni ya Watanzania wote, hivyo hatupaswi kulazimishana au kukatishana tamaa.

Viongozi wetu pia wanatakiwa kuwa na kauli zinazofanana kwa nia njema, ili tunaongozwa au kuwakilishwa, tuwafuate na tusaidiane kuijenga nchi yetu, badala ya kuiacha rehani kwa watu wengine bila kuangalia ni upi mustakabali chanya wa nchi. **Alamsiki**!

# HABARI PICHANI



Mkaguzi wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Hebert Kazonde, akisimamisha pikipiki ya kubeba mizigo ya miguu mitatu jana katika eneo la stendi kuu ya mabasi Muheza kwa ajili ya ukaguzi wa makosa mbalimbali ikiwamo leseni ya udereva. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Gabriel Migire (kulia) akibadilishana hati za makubaliano na Katibu Mkuu wa Wizara ya Usafirishaji wa Umma wa Malawi, Hasting Chiudzu, kuhusu ushirikiano katika usafiri wa njia ya barabara, huduma za bandari katika Ziwa Nyasa na uhudumiaji wa mizigo ya Malawi kupitia bandari ya Dar es Salaam. **PICHA: WUU.**




Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma juzi kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya wakala na mwelekeo wa Mwaka wa Fedha 2023/24. **PICHA: PAUL MABEJA.**



Sehemu ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Msalato mkoani Dodoma, kama ilivyokuwa juzi. **PICHA: WU**




Mjasiriamali akisukuma mkokoteni akitafuta wateja wa kuwauzia miwa katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAISHA

JUMAPILI AGOSTI 20, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

**Rosti maini ya kuku**





Ukurasa 14

## MITINDO:
UBUNIFU HUU HATARI



## JE UNA TUMIA BOMBA LA MVUA?

Ukurasa 15




# USO ULIONG'ARISHWA

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | | K | I | A | Z | I |
| H | | | | M | | M |
| I | | J | A | A | | K |
| M | I | A | | N | O | A |
| B | | M | L | A | | N |
| U | | B | | | | D |
| A | K | O | M | E | | E |

## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU, TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU, JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 2 | | 3 |
| | 3 | | 4 |
| | | | 1 |
| | 1 | 4 | |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


ZAO, NTA, GAO, JAA, OGOPA, GONGA, ZONGO, NGOJA, AMKANYE, TANGAZO

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

Mtoto Juma alikwenda mtoni na mama yake kuchota maji.

Wakati wakichota maji, Juma aliona kiota cha ndege kikielea majini.

Haraka Juma alimuonyesha mama yake na kumuuliza

Juma; Mama ona kile kinachoelea majini

Mama: Ni kiota cha ndege kile nadhani kimeanguka majini.

Juma: Mama yani hata kiota kimeundwa? Mwalimu wetu alituambia kuwa kila kieleacho majini kimeundwa.

Mama: Ni kweli lakini ina maana zaidi kuwa kila kilicho bora kuna jitihada zimetumika.

Swali

Mnyama gani mwenye damu baridi anayeishi mtoni.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Je, umewahi kusingiziwa mchawi?

KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Bila shaka unajifunza kitu kupitia mada ninazowasilisha hapa. Wiki iliyopita niliahidi kujadili kisa cha mwanaume anayeteswa na mama mkwe wake. Bado nakifanyia utafiti nikikamilisha nitakileta hapa.

Leo tuangalie mbinu anazotumia shetani kushambulia wanawake, iwe wameolewa au hawajaolewa. Shetani katika vita dhidi ya mwanamke ametengeneza mbinu ili amshambulie, lengo likiwa ni kumvunja moyo, kumuumiza na kuua hatma yake.

Moja ya mbinu ikiwa ni kuwatupia roho ya kichawi. Uchawi ni silaha kubwa anayotumia shetani ili kuwaangamiza wanadamu.

Wengi wetu tutakumbuka serikali yetu miaka ya nyuma ilivyopambana sana na watu waliokuwa wakiua wanawake vikongwe hasa kule Shinyanga kwa kusingiziwa ni wachawi. Ilikuwa ni janga kubwa la kutia hofu katika taifa letu.

Uchawi ni silaha ya uharibifu inayotoka kuzimu ikiwa na lengo la kuua na kuangamiza wanadamu. Ni nguvu ya kufanya uovu na kuharibu mema. Ni roho inayopindisha hatma ya mtu. Ni roho inayokandamiza na kumtawala mtu.

Uchawi ni roho (nguvu) ya uharibifu toka kuzimu inayowavaa wanadamu ili kumuangamiza yeye na wanaomzunguka. Mchawi ni mtu aliyepagawa na roho ya kichawi. Roho hii imeleta uharibifu mkubwa sana kwenye ulimwengu tunaoishi.

Uchawi haujaanza siku hizi, bali ulianza zamani sana kwenye nyakati za uandishi wa vitabu vya dini. Hii ni maelfu ya miaka, zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

Hata hivyo, imebainika kuwa uchawi upo sana kwa wanawake. Na kwa sababu ya roho hii ya uchawi, wanawake wengi wanaishi maisha mabaya sana.

Msomaji wangu, zipo aina 3 za kumilikishwa uchawi. Na ikumbukwe kwamba siyo kila mtu anayeitwa mchawi ni mchawi. Wengine wanasingiziwa na kujikuta wakipata madhara makubwa wasijue cha kufanya.

Kwanza, yupo mchawi anayejifahamu. Labda tu baada ya kuingia kwenye kikosi anashindwa kujinasua kirahisi. Wachawi ni mawakala wa shetani wanafanya kazi kwa niaba a shetani, wakilenga kuharibu kabisa uumbaji wa Mungu.

Hawa ni watu ambao aidha walirithishwa na wazee wa ukoo wakaukubali, au waliamua kumiliki kwa hiari yao wenyewe. Wengine husafiri mbali kutafuta na kununua uchawi kwa gharama zao wenyewe. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Mwingine ni mchawi asiyejifahamu. Hili ni kundi linalotumiwa na shetani pasipo wao kujifahamu, na ni asilimia kubwa sana ya watu wa jinsi hii. Watu wa aina hii hutumikishwa pasipo wao kujifahamu na ni kinyume na mapenzi yao, lakini hawana nguvu za kujitetea!

Watu hawa mara nyingi huota ndoto mbaya za kutisha pasipo wao kujua kuwa wanatumikishwa kichawi. Upo wakati mtu atamuota mtu fulani akiwa mtupu bila nguo anamfanyia mambo ya kichawi.Tatizo hili limefanya hata watu wengine kuuana.

Kwa hiyo, mtu anaweza kuchukuliwa hata sura yake na akatumiwa kwa njia za kichawi. Mara nyingi wale wachawi wanaojifahamu ndio hutumia sura za watu ili kufanya kazi zao za kichawi.

Na wao wanakuwa wamejificha na huku watu wasio na hatia ndio wanaonekana wao ni wachawi. Ni muhimu sana tuwe makini na mbinu hizi chafu za kichawi, vinginevyo, jamii zetu zinaweza kufarakana kwa kiwango cha kutisha!

Pia yupo mchawi aliyelazimishwa. Hawa ni watu ambao hawapendi kufanya uchawi, lakini wanalazimishwa na kama hawatafanya hivyo adhabu kali ingetolewa kwao.

Wengine wanajikuta wamelazimishwa kuwa wachawi wakiogopa kuuawa. Upo uovu/uchawi ambao watoto wadogo hasa wanaoambukizwa kupitia pipi, biskuti kutoka kwa wanafunzi wenzao mashuleni.

Na wanaporudi nyumbani tayari wanakuwa wameshabadilika na kuleta uharibifu na ugomvi ndani ya nyumba. Mtoto wa aina hii akiombewa na Mtumishi wa Mungu mwenye nguvu ya kufichua, adui hulipuliwa na kumwachia.

Mama mmoja rafiki yangu pale Kimara DSM aliniambia siku moja wakiwa wamelala, alishtuka usingizini majira ya saa saba usiku. Alipogeuka hakumuona mwanaye mwenye umri wa miaka minne pembeni mwake.

Alipotupa macho akamuona amesimama mlangoni anachezesha miguu kama anacheza gwaride. Akamfuata akamsemesha mtoto akashtuka. Ndipo akamrudisha kitandani.

Alipomsimulia jirani akamwambia wapo wachawi huchukua watoto kichawi kuwatumikisha au kuwachezesha ngoma usiku.

**Wiki ijayo tutaangalia maeneo mengine shetani anayotesa nayo wanawake. Una kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Vitanzi ni ukatili mpya wa kunyimana tendo la ndoa?

UZAZI wa mpango ni uamuzi wa hiari wa mtu binafsi mke na mume au mtu na mwenzi wake kuhusu lini waanze kupata watoto, wazae wangapi, wapishane kwa muda gani, lini waache kuzaa na njia gani ya uzazi wa mpango wangependa kutumia. Wote tunakubaliana katika hilo.

Hakuna ubishi kwamba ni muhimu kwa anayetaka kutumia uzazi wa mpango kufanya tathmini ya kina juu ya usalama na ufanisi wa kila njia kwa sababu si kila njia ya uzazi wa mpango inamfaa kila mtu, kila mtu ana njia yake kulingana na mazingira.

Huwezi kuamka tu na kwenda hospitalini unasema unaenda kuchoma sindano, kuweka kitanzi, kipandikizi au vidonge.

Sharti kwanza, ujue njia zote na faida yake na kisha upime kulingana na umri na mazingira yake njia ipi itakufaa.

Nimesukumwa kuandika waraka huu ili kuishtua serikali na mamlaka zake, kuyatazama malalamiko ya wananchi wa Mwika Kusini, huko wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wanaolalamika wenza wao kuwafanyia ukatili kwa kuwanyima tendo la ndoa kwa sababu hawana pesa ya kuwahudumia.

Wamepaza sauti zao katika vyombo vya habari, kupitia mdahalo wa jamii uliokuwa ukijadili nguvu ya uwezo wa wanawake kusaidia kumaliza matatizo ya ukatili wa kijinsia katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa kushirikiana na wanawake wanaharakati.

Katika mdahalo huo uliendeshwa na Shirika la KWIECO kwa kushirikiana na Women Fund Tanzania Trust (WFT-Trust), wamelalamikia kukithiri kwa vitendo vya ukatili wa kingono, hasa ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto, lakini pia wanawake kunyimwa haki ya kurithi mali.

Achilia mbali vipigo na ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanaume kutajwa kuwa miongoni mwa matukio ya ukatili yanayoendelea kuota mizizi katika kata hiyo; chanzo ni wazazi kutokutimiza wajibu wao wa kutunza familia, ulevi uliokithiri, kutokuwa na elimu ya masuala ya haki za binadamu na matukio ya ukatili kutokushughulikiwa ipasavyo na vyombo vya dola.

Kubwa zaidi, wanaume wameeleza masikitiko yao kuhusu baadhi yao kufanyiwa na wenza wao ukatili kama kuwanyima 'unyumba' kwa sababu hawana pesa ya kuwahudumia.

Kibaya zaidi ni namna wake zao wanavyotekeleza kile walichokiita ukatili wa kisaikolojia dhidi yao, kwa kuweka vipandikizi vya uzazi wa mpango ili kuwazuia wasizae nao.

Tazama kauli hizi zinavyoumiza wanaume: "Unazungumza nini! sasa hivi watoto wako huku (anaonyesha kwa kupiga kwa mkono bega lake), nani ana muda wa kuzaa? Wanawake wanasema hawana muda wa kuzaa, wana muda wa kutafuta pesa.

"Nazungumza ukweli na nyie kina mama mjue na Mungu anasikia. Wanafungia watoto huku (begani), hata ufanyeje hakuna mimba. Nyie akina mama muangalie mpange muda wa kuzaa kuongeza taifa."


Baada ya kauli hiyo, mwanamke mmoja jasiri akasimama akajibu: "Hatutaki kuzaa kwa sababu tunalea peke yetu. Nina mume ninabeba mimba peke yangu miezi tisa, naenda leba najifungua pale. Wakuja kuniangalie pale hakuna, natoka hospitali narudi nyumbani natakiwa nile uzazi miezi mitatu, wa kuniangalia kwenye ule uzazi hakuna.

"Mtoto anakua anatakiwa malazi, anatakiwa elimu, haki zote za mtoto anatakiwa na anayezifanye zote ni mimi mwanamke. Nimeshazaa mtoto wa kwanza nimekiona, nimezaa wa pili nimekiona, hivi kweli nitathubutu kuongeza wa tatu na wa nne? Kwa hiyo ziko sababu zinazotufanya wanawake na mabinti tunaokua tutumie uzazi wa mpango."

Kwamba sasa hivi eti wanawake wa Uchagani hawaelewi somo, wameziba masikio na kwao ni mwendo wa matumizi ya sindano, vidonge, kitanzi na kutoshiriki ngono na waume zao.

Amkeni ninyi maofisa ustawi wa jamii, maofisa maendeleo ya jamii, Wizara ya Afya na Wizara husika ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya afya ya afya ya akili yanayosababishwa na kukithiri kwa ukatili wa kijinsia.

• **Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**











Waigizaji nyota wa filamu za Bongo Muvi, Shamsa Ford na Husseni Lugendo maarufu kama Mlilo, hatimaye wamefunga ndoa juzi. Harusi hiyo ilifanyika nyumbani kwa baba mdogo wake Shamsa, Tabata Kinyerezi, jijini Dar es Salaam.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



## UBUNIFU HUU HATARI

WANAMUME wanatakiwa kuwa makini katika kufanya chaguo sahihi la mavazi ili waendane na mazingira ya kisasa.

Tabia za kutojali sana kuchagua nguo zinazolingana na hitaji la mwili wake, inawafanya kutokuwa maridadi kutokana kuvaa nguo tofauti na mwonekano.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanashauri utanashati wa mtu ni pamoja na umakini wakati wa kununua mavazi.

### JINSI YA KUCHAGUA

Kama wewe ni mvivu kununua nguo, hakikisha unanunua mavazi ya rangi nyeusi kwa sababu yana kawaida ya kutochosha muonekano wa mtu.

Mwanaume anapovaa suruali nyeusi haitaji kufikiri sana kuhusu rangi ya shati, viatu au fulana.

Suruali nyeusi haichagui rangi ya vazi au nguo yoyote inayoambatana nayo.

Unashauriwa kuchukua suruali yenye kubana kiasi kwa sababu unapovaa na shati muonekano wako unakuwa wa kipekee.

### VIATU

Suruali nyeusi inafaa sana kuvaliwa na viatu vya rangi nyeusi, udongo au nyeupe iliyofifia.

Hata hivyo wengine wanapenda kuvalia viatu vya wazi vya rangi yenye mng'aro dhaifu na wanatoka bomba.





URE MBO

Na Mary Geofrey

# USO ULIONG'ARISHWA



WATU wengi wanatumia mafuta ya aina tofauti yenye viambata vya sumu kama njia ya kung'arisha uso.

Hata hivyo mafuta yenye kemikali mengi yana kawaida ya kuharibu ngozi na kusababisha uzee.

Hata hivyo, wataalamu wa urembo wanashauri njia za asili za kung'arisha na kuondoa vipele kwa gharama rahisi.

**Kipande cha barafu**

Barafu husaidia kukausha au kunyausha chunusi, kunyonya mafuta na kuyasambaza katika maeneo mengi ya mwili.

Chukua barafu tia kwenye kitambaa safi anza kufanya kama una sugua taratibu sehemu yenye chunusi, rudia hivyo mara nyingi. Asali

Imethibitishwa na wataalam wa ngozi kuwa asali inasaidiaa sana kuondoa chunusi kwa kuzibua matundu ya hewa ya ngozi na kufanya ngozi kupumua vizuri.

Tumia pamba safi chovya asali paka katika eneo lenye chunusi fanya kama unakanda eneo husika, acha kwa dakika 10 osha kwa maji ya uvuguvugu.

**Maji ya limao**


Limao linaua vijidudu katika ngozi, pia huondoa chunusi haraka kwa sababu ya kemikali zipatikanazo ndani yake

Tumia pamba safi weka kwenye eneo lenye chunusi baada ya hapo lala mpaka asabuhi , nawa uso wako.

**Dawa ya Meno**

Dawa ya maajabu ya kuondoa chunusi haraka bila kuacha kovu, inakausha chunusi haraka sana.


Chukua dawa kidogo weka eneo lenye chunusi mpaka asubuhi kisha nawa uso kwa maji safi.



**Kitunguu Swaumu**

Kitunguu hutibu magonjwa takribani 20 pia chunusi kwa uharaka sana.

Kata kitunguu swaumu vipande viwili sugua taratibu eneo lenye chunusi.



**Chapa maandashi**

Pia namna nyingine ya kuondoa chunusi, inasaidia kunyonya mafuta usoni haraka sana na kuacha uso ukiwa mkavu na nyororo.

Weka kijiko kimoja cha chai kimoja cha chapa maandashi.

Maji kiasi au maji ya limao, changanya, osha uso wako vizuri kisha paka mchanganyiko wako na subiri kwa dakika tano kisha uoshe.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Rosti maini ya kuku

LICHA ya utamu wake, watu wanahofia kupika maini ya kuku kwa sababu ni laini.

Usihofu hata kidogo, kwani unaweza kujifunza na kupika kwa ustadi bila kulainika na kupoteza mwonekano wake.

**Mahitaji**

Maini ya kuku nusu kilo, vitunguu vikubwa viwili, hoho moja, pilipili moja, limao nusu kipande, Swaumu na Tangawizi kijiko cha chai kimoja.

Curry powder nusu kijiko cha chai, chumvi na mafuta ya kupikia.

**Matayarisho**

Safisha maini weka pembeni. Baada ya hapo kaanga vitunguu,swaumu na tangawizi pamoja (hakikisha vitunguu visiwe vya brown), kisha tia maini, curry powder, pilipili, chumvi ,hoho na limao.

Changanya vizuri viungo vyote na maini hadi vikae sawa na ufunike.

Pika mpaka maini yaive na hakikisha yanakuwa na rojo kidogo, usikae mbali kwa sababu ni laini yasije kupondeka.

Baada ya hapo ipua na hapo yatakuwa tayari kwa kuliwa na chochote upendacho kama vile chapati, chips, ugali na wali.



## MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# JENGA DARI BORA USIJE KUJILAUMU BAADAYE

KATIKA nyumba leo, tunazungumzia umuhimu wa kuzingatia umaliziaji mzuri wa dari kwenye nyumba.

Hii ni sehemu ambayo watu wengi wanaojenga nyumba zao husahau kuipa kipaumbele. Lakini msanifu wa nyumba, Kimboi Marick, anasema hiyo ni sehemu muhimu zaidi kwa sababu ndiyo hupendezesha zaidi nyumba.

Marick anasema dari katika ujenzi wa nyumba mara nyingi watu wengi hawaipi uangalizi mkubwa lakini ni sehemu ambayo isipomaliziwa vizuri, inaweza kuharibu kabisa kazi yote nzuri ya ujenzi wa nyumba iliyofanyika.

Pia anasema kwa sababu inaficha vitu vingi kwa ndani, endapo haitajengwa au kumaliziwa vizuri kitaalamu, inaweza kusababisha athari kubwa kwenye nyumba.

"Dari imekuwa sehemu ambayo inasahaulika sana katika ujenzi wa nyumba zetu kwa maana ya kuwa inapewa uangalizi kidogo sana lakini umaliziaji mzuri wa dari hii ndio unaozidisha uzuri wa nyumba yako. Inasaidia kuiweka imara na kwa usalama zaidi," anasema Marick.

"Dari ndio inaficha mabomba ya umeme na huduma zingine ikiwamo kuondoa uzia kwenye macho ya watu wanaoingia au kuishi kwenye nyumba husika na kuipa mwonekano mzuri. Ili upate faida zote za dari hii ni vyema kumpata fundi au msanifu mzuri wa majengo anayeweza kusimamia kazi hiyo kwa ufanisi unaotakiwa," anasisitiza

Anasema kabla ya kufanya uamuzi wa umaliziaji wa nyumba yako, ni vyema ujitafakari na kufanya uamuzi kwanza wa aina ya mwonekano wa dari unayoitaka kwenye nyumba yako ili kuepuka kujilaumu baadaye.

"Tafakari na uamue, unataka kupata mwonekano gani. Fanya uamuzi sahihi ni muundo gani wa dari unalolihitaji na usikurupuke ili ukajilaumu baadaye. Kumbuka kuna dari inayotakiwa kutengenezwa sebuleni, vyumbani, jikoni na hata vyooni. Na katika kila maeneo yote hayo unatakiwa kuamua.

"Unaweza kuamua mwonekano wa dari ya sebuleni ukawa tofauti na wa vyumbani au ukafanana. Hiyo yote itategemea na namna unavyopendelea wewe lakini la muhimu kuzingatia ni kwamba unatakiwa kuhakikisha unatumia watu ambao ni wataalamu ili walimalizie vizuri na kuiweka nyumba katika hali ya usalama zaidi," anamalizia.



## Je unatumia bomba la mvua?



**Na Restuta James**

MABADILIKO yanayoendelea kutokea kwenye nyanja mbalimbali yanaifanya sekta ya ujenzi kuonekana mpya kila siku.

Wataalamu wa mapambo ya ndani, samani na ujenzi kwa ujumla, wanayaeleza mabadiliko hayo kama mageuzi ambayo yanaenda kwa kasi kila siku.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, mtaalamu wa vifaa mabomba, Daniel Deogratius, anasema kumekuwa na uvumbuzi wa hali ya juu katika eneo hilo.


Anatoa mfano kwamba mabomba ya juu (shower mixer), ambazo zinatoa maji ya moto au baridi zimeboreshwa kiasi cha kumwezesha mtu anayeoga kuamua joto la maji analohitaji kutoka kwenye 'hitter'.

"Zimekuja za aina ya kipekee zenye kitufe cha kumwezesha mtu kupooza maji yake ya moto kwa joto analotaka na sio unaoga kwa kubahatisha. Zimekuja na vitufe maalumu kukuwezesha kupima joto la maji hata kabla hujaanza kuoga," anasema.

Daniel anasema awali, mtu aliweza kuchanganya maji kwa bomba la mvua kwa kuyapima kwa mikono kwa dakika kadhaa, jambo ambalo linatatuliwa na aina mpya ya 'shower mixer.'

"Hivi sasa unaona kwenye kitufe maalumu kwamba ukioga na maji haya yana nyuzijoto 20, 30, 10 au 100...hili unaliona hata kabla hujaanza kuoga," anasema.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

KIPIMO CHA KINGEREZA UKISHALEWA...

# Watu watano wauawa Ukraine

**KYIV,** UKRAINE
WATU watano wameuawa na wengine 37 wamejeruhiwa baada ya kombora lililorushwa na majeshi ya Russia kushambulia mji wa Chernihiv kaskazini mwa Ukraine.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ukraine ilisema kwamba watoto 11 walikuwa miongoni mwa waliojeruhiwa.

Kombora hilo lililenga jengo la chuo kikuu na ukumbi wa michezo.

Rais Volodymyr Zelensky, alichapisha video fupi ikionyesha magari yaliyoharibika na jengo hilo likiwa limeteketea na kujaa vifusi.

Mji wa Chernihiv uko karibu na mpaka wa Belarusi.

Wakati wa uvamizi mji huo ulichukuliwa na Russia, lakini ukatwaliwa tena na askari wa Ukraine.

"Kombora kutoka Russia lilipiga katikati mwa jiji letu la Chernihiv. Chuo kikuu cha polytechnic, na ukumbi wa michezo," alisema Rais Zelensky kupitia mtandao wa Telegram.

"Jumamosi ya kawaida, ambayo Russia imeigeuza kuwa siku ya maumivu na hasara. Kuna wafu, kuna waliojeruhiwa," aliongeza.

Aidha, Russia imedai kuwa ndege isiyo na rubani ya Ukraine iligonga uwanja wa ndege wa kijeshi kaskazini magharibi mwa mkoa wa Novgorod, na kusababisha moto ambao ulizimwa haraka. Ndege moja iliharibika lakini hakuna hasara iliyoripotiwa, iliongeza. Ukraine haijazungumza lolote kuhusu shambulio hilo.

Wakati huo huo, Marekani imeidhinisha kuhamishwa ndege za kivita aina ya F-16 zilizotengenezwa nchini humo kutoka Denmark na Uholanzi kwenda Ukraine.

Ukraine imesifu uamuzi huo ambao iilikuwa ikishinikiza kwa bidii tangu mwaka jana.

Inatarajiwa kuwa itachukua miezi kadhaa kabla ya Ukraine kuweza kutumia ndege hizo za F-16 na kukabiliana na ubora wa wanajeshi wa anga wa Russia.

Uholanzi inafikiria takriban ndege 24 za F-16 zinazofanya kazi ambazo zimeondolewa kazini na nafasi yake kuchukuliwa na ndege zenye uwezo wa juu.

Marekani na washirika wake hapo awali walikataa kutoa ndege hizo Ukraine, wakihofia kwamba hii ingesababisha kuongezeka kwa mashambulizi zaidi ya Russia.

**BBC**



Pichani moshi ukifuka katika majengo ya jiji la Khartoum kutokana na wapiganaji wa RSF na wanajeshi wa serikali kuendelea na mapigano. **PICHA: REUTERS**

# Kikosi cha kijeshi kiko tayari kuivamia Niger

**ACCRA,** GHANA
KIKOSI cha kijeshi cha Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) kimeelezwa kiko tayari kuivamia Niger.

Kamishna wa masuala ya kisiasa , amani na usalama wa jumuiya hiyo, Abdel - Fatau Musah, alisema inachosubiriwa ni amri kutoka kwa viongozi wanachama.

"Tuko tayari kuingilia kati mara tu amri itakapotolewa. Siku ya kuingilia pia imepangwa na inajulikana", alisema Musah.

Wakuu wa majeshi ya ECOWAS waliamua juu ya mbinu za uingiliaji kati kijeshi kama njia ya mwisho ya kumrejesha madarakani rais mteule Mohamed Bazoum ambaye alipinduliwa Julai 26 na wanajeshi.

Hata hivyo, walisisitiza tena kwamba ECOWAS inaweka mbele njia ya mazungumzo.

Hata hivyo ECOWAS ilitangaza ingetuma ujumbe wa kidiplomasia jana kwenda nchini Niger, wakati ujumbe wa awali ukishindwa kukutana na kiongozi mpya Jenerali Tiani.

"Tuko tayari kusuluhisha tatizo hilo kwa amani, lakini kunahitajika pande mbili kufikia suluhu," alisisitiza Musah.

Aliongeza "sisi hatutakuwa wa kubisha mlango wakati hawataki kufungua,"

Ilisema ikiwa jeshi la Niger linataka kuchukua njia ya amani ili kurejesha utaratibu wa kikatiba wako tayari kuacha chaguo la kijeshi, kwa sababu sio chaguo tunalopendelea, lakini watalazimika kufanya hivyo kwa sababu ya kuondoa utawala usio na usawa.

"Nchi zote wanachama wa ECOWAS walioko hapa (Ghana) wamejitolea kutoa wanajeshi, vifaa na uwezo unaohitajika kutekeleza azma hii," ofisa huyo alisema..

Mataifa yote wanachama wa ECOWAS yamewakilishwa katika mkutano huo, isipokuwa Cape Verde na Guinea-Bissau.

Kwa upande wa Guinea, Mali na Burkina Faso, zilisimamishwa kwenye bodi zinazosimamia ECOWAS kutokana na kungozwa na wanajeshi waliofanya mapinduzi.

**RFI**

# Mapigano yashika kasi Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN
MAPIGANO makali yanazidi kushika kasi nchini Sudani kati ya wanajeshi wa serikali na na wanagambo kikosi maalum cha uingiliaji kati (RSF).

Vita hiyo imesambaa katika maeneo ambayo yamekuwa na utulivu na kusababisha watu kukimbia makazi yao.

Wakazi wa maeneo ya Kusini mwa Sudan walisema tangu siku ya Alhamisi, makabiliano makali yamekuwa yakishuhudiwa katika mji wa El Fasher ambao umekuwa na utulivu kwa miezi miwili.

Hali kama hiyo pia inashuhudiwa katika jimbo la Kordfan Kaskazini, na kusitisha shughuli za usafiri.

Vita hivyo vimesababisha watu zaidi ya laki sita, kutoka jimbo la Darfur kukimbilia katika mji wa El Fasher, huku wengine wakikimbilia katika nchi jirani ya Chad.

Katika hatua nyingine, kundi la waasi la Tamazuj Front lililotia saini mkataba wa amani, limetangaza kujiunga na wanamgambo wa RSF.

**RFI**

# China yafanya mazoezi kijeshi karibu na Taiwan

**BEIJING,** CHINA
CHINA imezindua mazoezi ya kijeshi karibu na kisiwa cha Taiwan kama ishara ya onyo baada ya kuelezea kukasirishwa na ziara ya muda mfupi iliyofanywa na makamu wa rais William Lai, nchini Marekani.

Lai, ambaye ni mgombea anayeongoza katika kura ya maoni katika uchaguzi wa rais wa Taiwan utakaofanyika mwakani na pia ni mkosoaji mkubwa wa China.

Wakati akirejea nyumbani kutika ziara yake nchini Paraguay, alisimama kwa muda mjini New York na San Francisco.

China iligadhabishwa na hatua hiyo ya Lai na kuelezea kwa mara nyingine kwamba mwanasiasa huyo ni msumbufu na kuapa kuchukua hatua kali.

Taiwan kwa upande wake imethibitisha taarifa za China kufanya mazoezi ya kijeshi, ikisema ndege za kivita zipatazo 42 zimeshuhudiwa zikipita katika anga lake.

Wizara ya ulinzi ya Taiwan imelaani mazoezi hayo ya kijeshi ya China na kuyataja kuwa ni tabia ya kichokozi.

**DW**

## MAKALA

# WENYE NISHATI MBADALA WAUNGWE MKONO



Na Magabilo Masambu

**Munuo anasema ikiwa atafunga mtambo wa kuzalisha nishati hiyo, utadumu zaidi ya miaka 30 na ubadilishwaji wa malighafi zinazotumika unaanza baada ya miaka minne toka mara ya kwanza ulipofungwa na uzuri wake mwingine ni kwamba ile taka inayotolewa kwenye mtambo baada ya kutumika, inakwenda shambani kama mbolea safi kabisa isiyo na wadudu kwa maana nyingine hakuna kitu cha kupoteza.**

"NILINDE nikulinde." Hivi ndivyo mazingira yanaweza kutwambia sisi binadamu na wanyama. Ukweli kwamba maisha yetu yanategemea mazingira yanayotuzunguka halitaweza kupingwa na yeyote. Kwa hiyo ni muhimu juhudi kubwa katika shughuli zetu za kila siku, tuhakikishe tunayalinda mazingira ili yaweze kutulinda pia. Uharibifu wowote wa mazingira ni uharibifu wa maisha yetu na viumbe vyote vinavyoyategemea.

Katika sikukuu za Nanenane, niliona jinsi Watanzania wengi walivyobuni teknolojia mbalimbali ambazo zinakusudia kulinda mazingira yetu. Wako wengi sana lakini nani anaona ujuzi wa watanzania hawa?

Nani yuko tayari kuwasaidia ili kuwafikia watu wengi zaidi? Au tunafanya kazi ya kwenda kutazama na kuwasifu, kisha mpaka Nanenane ijayo? Ni muhimu kuonyesha tumeona na tunajali kazi zao na kama haitoshi tuwasaidie kwa namna mbalimbali, ili kuweza kuyaokoa mazingira yetu na tuishi vizuri.

Serikali imekuwa kila wakati ikipambana na wanaotumia kuni pamoja na kuchoma mkaa kwamba wanaharibu mazingira. Ni kweli lakini watumie nini na wanahitaji kula ili waishi? Kuna wakati tumeona waziri wa nishati mahala fulani akigawa mitungi midogo ya gesi katika maeneo ya vijijini, lakini unajiuliza hivi kwa familia zilivyo kubwa katika maeneo ya vijijini ule mtungi wa gesi unatumika siku ngapi? Na je iwapo gesi itaisha, watakuwa na uwezo wa kununua nyingine kwa vipato vya wakulima wanaotegemea mazao ya msimu?

Ni jambo linalofikirisha kidogo na katika kufikiri huko, nadhani ni muhimu kutafuta njia za kudumu na za muda mrefu zenye gharama ndogo kwa watumiaji. Mfano kama gharama za umeme zingekuwa chini zaidi na zikawafikia wananchi mpaka vijijini, matumizi ya mkaa na kuni yangekuwa historia. Lakini kwa sababu bado tumo katika juhudi hizo, basi wale wanaojitokeza kutafuta njia mbadala tuwafahamu na tuwasaidie, ili tusijikute umeme unafika kila kijiji lakini hatuna miti hata ya vivuli.

Suzana Fred Munuo ni binti ambaye amejizatiti katika kutumia taka, mabaki ya chakula au vinyesi vya wanyama katika kutengeneza nishati mbadala ambayo ni rafiki kwa mazingira na kwa watumiaji. Inawezekana teknolojia hii si ngeni lakini kila mtu ana namna anavyoweza kuifanya itumike kwa urahisi. Kilichonivutia zaidi ni kwamba ukiachana na matumizi ya vinyesi vya wanyama ambavyo wakati fulani vinaweza kuwa adimu kwa mtumizi ya mbolea, lakini kutumika kwa mabaki ya vyakula na takataka za sokoni ambazo nyingi hukusanywa na kutupwa kwenye madampo ya taka maana yake ni kwamba itakuwa njia rahisi sana ya kuyafanya mazingira yawe safi wakati teknolojia kwa upande mwingine, ikilinda mazingira kwa kuacha kutumia kuni na mkaa.

Munuo anasema ikiwa atafunga mtambo wa kuzalisha nishati hiyo, utadumu zaidi ya miaka 30 na ubadilishwaji wa malighafi zinazotumika unaanza baada ya miaka minne toka mara ya kwanza ulipofungwa na uzuri wake mwingine ni kwamba ile taka inayotolewa kwenye mtambo baada ya kutumika, inakwenda shambani kama mbolea safi kabisa isiyo na wadudu kwa maana nyingine hakuna kitu cha kupoteza.

"Changamoto yangu kubwa ni kwamba Watanzania wengi bado hawajawa na elimu juu ya teknolojia hii lakini ikiwa itawafikia tunaweza kuokoa mazingira kwa upana wake. Sasa hivi unaona hata majira ya mvua yamebadilika watu sasa hawazalishi hata mazao ya chakula tu ikiwa mwendo utakuwa ndiyo huu huko mbeleni kutakuwa na hatari kubwa ya kukosa chakula. Lakini sababu kubwa na ya msingi ni juu ya uharibifu wa mazingira.

"Ombi langu kwa Waziri wa Nishati, January Makamba, anisaidie tu Watanzania wengi waifahamu hii teknolojia maana vita ya mazingira ni kubwa. Lazima tupigane pamoja kuhakikisha watu wananufaika na ubunifu hu tunaoufanya, mwisho wa siku tuwe na Tanzania salama kwa binadamu na viumbe wengine," anasema.

Loishiye Lenoy Mollel, makazi wa Arusha, ni miongoni mwa watumiaji wa teknolojia hiyo na anakiri kwamba tangu awe mtumiaji wa nishati hiyo hajaona tatizo lolote na sasa ana miaka miwili bado hajabadilisha malighafi zilizotumika. Hana haja ya kutumia mkaa wala kuni ten ana rai yake ni kwamba ikiwa Watanzania wengi watafikiwa na elimu hii watasaidia sana kulinda mazingira katika maeneo yao.

"Hii nishati naona kama nilichelewa kuifahamu maana kwa kweli tumenufaika kwa mengi. Kwanza stumii tena gharama za kununua mkaa lakini sasa nalinda mazingira kwa kutotumia kuni na mkaa," anasema.

Ushauri wangu kwa serikali ni kwamba tuwasaidie Watanzania wenzetu wanaoonyesha uwezo wa kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Kamwe hatutaendelea kwa kutegemea wawekezaji kutoka nje. Wao wanakuja kutengeneza faida na kuhamisha mitaji lakini wa hapa kwetu faida yao inabaki hapa hapa. Tusijione hatuwezi, tukipunguza uwekezaji wa watu kutoka nje tutawakuza hawa wa kwetu na mwisho watasimama na kuajiri watanzania wenzetu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mwanamume aliyeomba muda akajinoe ili kulishika penzi*



Na Adam Fungamwango

YEYOTE aliyetendwa huwa mgumu sana kuingia tena kwenye mapenzi kwa mara nyingine. Kama atakubali kuingia tena, safari hii atakuwa mwangalifu sana na hatoingia tena kichwa kichwa kama mwanzo. Huwa anayafikiria maumivu aliyoyapata baada ya kuachana na mpenzi wake wa mwanzo kwa sababu ya kusalitiwa au kuachwa.

Atachukua muda mrefu kwanza kuangalia na kumchunguza ambaye anataka tena kujenga naye uhusiano.

Awali kabisa, yeyote aliyetendwa maumivu anayoyapata ni makubwa mno kiasi kwamba anaapa kutopenda tena.

Kama mwanamume, ataona kila mwanamke anayemsogelea ni wale wale tu.

Mwanamke naye ataona wanaume wote ni kama wamezaliwa na baba mmoja. Kila anayemfuata kutaka kujenga naye uhusiano anaweza kuambulia maneno makali, kejeli na matusi kiasi kwamba mwanamume atashangaa ni kitu gani kimempata mwanamke yule.

Kumbe kisaikolojia anaongea au kujibu mambo yale yale ambayo mpenzi wake wa zamani alimfanyia. Kichwani kwake hamwoni mwanamume mwingine mpya, bali ni yule yule.

Anachoona ni kwamba anafuatwa ili afanyiwe kile ambacho alitendewa mwanzo.

Mara nyingi ukishayapata maumivu ya mapenzi, unakuwa mwangalifu sana kwani hakuna yeyote anayetaka kuyapata kwa mara ya pili.

Leo tunarudi tena kwa mwanamuziki Harila Tongilanga aliyevuma miaka ya 1980 akiwa na CTU Les Mwenge na baadaye Makondeko Six Band mwanzoni mwa miaka ya 1990, kabla ya kuunda bendi yake mwenyewe aliyoiita Makondeko Group Band mwishoni mwa miaka ya 1990 hadi anafariki dunia 2017 kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam.

Wiki mbili zilizopita tulikuwa na wimbo wake uitwao 'Saidaru' lakini leo tunautazama wimbo uitwao 'Nuru.'

Ni wimbo unaomzungumzia mtu mmoja ambaye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanawake mbalimbali, lakini kumbe hawakuwa na mapenzi ya kweli bali kuna kitu walikuwa wanakitafuta.

Alikuwa anaishi nao kwa muda mfupi wanamwacha na majonzi. Hali ilivyoendelea akaamua kuachana na mapenzi. Akaona tu bora 'ainjoi' kama anavyosema Jux katika wimbo wake 'Enjoy.'

"Bora niinjoi, maisha mafupi ni simpo, ya nini niteseke roho? Jiunge nami upoze koo."

Jamaa anaamua kuachana kabisa na mambo ya mapenzi, akajikalia tu 'anainjoi.'

Kama ilivyo kawaida ya kitu mapenzi, huwa kinakuja tu ghafla na hakijulikani kinatoka wapi.

Akakutana na dada mmoja anaitwa Nuru. Moyo ukampaa. Akampa ya moyoni, binti akakubali. Lakini jamaa anakumbuka alivyotendwa na kundi la wanawake waliopita mikononi mwake ndipo akaanza kuongea maneno yaliyomo mwenye wimbo huo.

"Najihofu kwa haki yangu kisicho kweli kwa mapenzi, ijapokuwa ninakupenda oo Bi. Nuru ee, moyo nao unanisuta huenda mapenzi sijui ikawa chanzo kinachowatoa warembo kwangu ooo Bi. Nuru eee, vuta subira sherii wako wenzio wa hali yako waliniacha, uzuri wako kisebusebu napata, nipe muda nipate hakika wewe ni wangu ee."

Anamwambia japokuwa anampenda sana ana wasiwasi kwa sababu alishakuwa na warembo wengi lakini walimwacha. Sababu haijui, labda mapenzi hajui, hivyo hata ukakika kama naye Nuru anaweza kukaa kwake, hivyo kwanza ampe muda awe na uhakika wa kile alichomjibu kuwa amemkubali.

"Wale wenzio wa hali yako waliopita wakilia, machozi yao yaliniosha nikawa nikawalilia ee, huruma ya macho usoni pao zilinichoma moyoni ikawa laini kwa kila jambo kuwakubalia ee, ooo Bi. Nuru ee chondechonde nakuomba, nipe muda nikajinoe nilishike penzi ee, kuna kitu mafichoni kwenye hili penzi lako nikikukosa nisiwe yatima wa kimapenzi eee."

Jamaa anamwambia mpenzi wake mpya kuwa warembo wengi aliowapata awali walionekana kama wana wapenzi wa kweli na wameumizwa walipotoka, hivyo aliwahurumia na kuwapa hifadhi na ikawa laini kwa kila jambo wanalotaka kuwatimizia, kinyume chake wakamkimbia, hivyo anamuomba Nuru ampe muda ajinoe, ajifikirie kabla ya kulishika penzi, ingawa anampenda lakini hofu ya kilichompata kwa waliopita ndicho kinachomtisha.

"Hakika ninavyokupenda Nuru ee, moyoni napata mcheche kwa mawazo nahofu ukija nisaliti Nuru ee, usije ukawa mwisho wangu dunia kuwepo."

Kwenye 'korasi' hii ndipo kuna msingi mkuu wa yote. Ni kwamba mwanaume huyu anampeda sana Nuru, lakini kilichomkuta nyuma kwa wanawake wengine ndicho ana wasiwasi nacho.

Anahofu kama ikija siku akimsaliti inaweza ikawa mwisho wake duniani kwa sababu maumivu atakayoyapata yanakuwa makubwa zaidi akiunganisha na yaliyomtokea huko nyuma.

Alijitahidi kukaa bila mpenzi lakini imetokea kwa kumpenda Nuru. Anahitaji muda wa kumsoma vizuri mpenzi wake ili awe na uhakika kuwa ni wake kabla ya kujiingiza mzima mzima kwenye penzi. Huyu ndiye Harila Tongolanga.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie kwenu-7

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AKAKARIBISHWA varandani na kushuhudia hali halisi ya nyumba ya wanawake warembo jinsi ilivyo.

Ilipambwa kwa mapambo mbalimbali ya kisasa, makochi, meza, viti, meza ya kulia chakula, shefu ya kuweka viatu na vitu vingine vingi vilivyomshangaza na kumfurahisha.

Kukaribishwa na mwanamke mrembo kama yule, tena varandani na siyo nje kwa mtu kama yeye ambaye amekuwa akiandamwa na matukio ya unyanyapaa, ilimfariji kwa kiasi kikubwa.

Wakati akiwa amesimama akishangaa uzuri na ndani humo pamoja na nakshi za taa, akakaribishwa kwenye kochi. "Kaa kwenye kochi James unasimama mtu mgonjwa kama wewe, utaanguka..." "Ahsante dada Carry." Mwenyewe aliingia chumbani na kukaa kiasi cha dakika 10 hivi, akatoka. Alikuwa amebadilisha nguo. Wakati huu alikuwa amevaa simpo tu.

Kitu ambacho muda wote alikuwa akiwaza James kama Carry yupo au hajarudi. "Catty yeye hajarudi?" Akauliza.

"Mida ambayo mimi natoka kazini yeye ndiyo anaingia. Vipi umemkumbuka rafiki yako?"

"Hapana nauliza tu."

"Enhe rafiki yangu sasa hebu niambie, hospitali wamekwambia kutibiwa ni shilingi ngapi?"

"Elfu kumi na tano, yaani sindano tano ambazo natakiwa kupiga kila siku moja na dawa."

"Catty akaweka mezani mkoba wake ambao walikuwa ametoka nao chumbani. Akaingiza mkono na kutoa noti mbili za shilingi elfu kumi akampa. "Hii hapa pesa ya matibabu, rudi leo hii hii ukaanze sindano na kutumia dawa, malaria ni ugonjwa mbaya sana, unahitaji matibabu ya haraka."

"Da' ahsante sana dada yangu."

"Halafu unasikia James, elfu tano iliyobaki ununue chakula ule kabla ya kutumia dawa, tena mgonjwa wa malaria unatakiwa ule sana, usitumie dawa kabla ya kula. Ungekula hapa, lakini bahati mbaya na mimi ndiyo kwanza naingia, hakuna chakula humu ndani. Na hiyo siyo ya mkopo, nimekupa ili usipate tabu ya kuanza kupita huku na huko unatafuta pesa wakati ni mgonjwa."

Wakati akiongea hayo alichukua simu yake na kupiga simu.

"Nilikwambia nitakupigia baadaye, njoo umchukue huyu kaka tuliyemkuta pale kwenye mti umpeleke




zahanati yeye mwenyewe yupo hapa atakwambia ni sehemu gani. Umpeleke na kumrudisha, sawa." Akakata simu.

"Yule dereva bajaj anakuja kukuchukua, utakwenda naye huko zahanati ili ukalipe na kupata matibabu. Halafu atakurudisha hapa kabla hujaenda nyumbani kwako upitie kwanza hata."

James ni kama vile alitamani ambebe Catty. Msichana mzuri, roho yake ni kama sura yake. Kila alichotaka kuongea cha shukurani aliona kama hakifai. Akajikuta akimwambia.

"Ewe msichana mzuri, sura yako ni kama roho yako, nipe shukurani nikushukuru unavyostahili kushukuriwa."

***************************

Majira yalionyesha ni saa nne asubuhi, lakini kulikuwa na joto kali. Ilionekana kama ni saa sita au saba mchana jinsi jua lilivyokuwa likichoma.

James alijizoazoa kwenye kibanda chake ili kujikongoja kwenda nyumbani kwa kina Catty kama alivyoambiwa.

Baada ya kutoka zahanati jana yake, akipata matibabu ya sindano mbili kwa mpiga na dawa alipolipa pesa aliyopewa na Catty alirejea tena nyumbani kwake.

Alikuta bibie alipika wali na samaki. Akampakulia na kumuwekea mezani.

"Kula mgonjwa, nimekuwekea na chachandu, maana mtu ukiumwa malaria kula chakula bila ndimu pilipili inakuwa utata." Catty alimwambia na akakaa pembeni yake akimpiga kampani na kumlazimisha kula hadi alipomaliza.

**"Kula mgonjwa, nimekuwekea na chachandu, maana mtu ukiumwa malaria kula chakula bila ndimu ndimu pilipili inakuwa utata." Catty alimwambia na akakaa pembeni yake akimpiga kampani na kumlazimisha kula hadi alipomaliza.**

"Kesho uje, usihofie kitu, utakula hadi utakapopona sawa?" James alimuitikia Catty "Ahsante dada."

Kabla ya kwenda huko alihakikisha anaenda kuoga na kupiga mswaki, ikiwa pamoja na kubadilisha nguo zake.

Alipohakikisha kuwa yuko sawa, alitoka nje, akafunga mlango wake na kuvuta hatua moja baada ya nyingine kuelekea anakokwenda.

Hakukuwa mbali sana. Ilikuwa ni kama unapandisha tu kilima hivi, unakata kona na nyumba ya tano ndiyo aliyokuwa akiishi Carry na ndugu yake Catty.

Akagonga geti na kufunguliwa. Aliyefungua alikuwa na Catty mwenyewe.

"Karibu James."

"Ahsante sana dada."

"Unasikiaje leo?"

"Yaani Catty, nashukuru sana dada yangu, leo angalau najiona kama binadamu."

Jibu lilimchekesha Catty, akamwambia," kwani mwanzo ulikuwa unajiona kama nani?"

"Nilikuwa najionea hivyo hovyo hovyo tu, hata sijielewi duniani sipo ahera wananitafuta."

Catty akafurahi tena kwa kicheko.

"Kumbe na wewe ina maneno ya chini chini wewe. Haya pita ndani, chai ipo nikakununulie kitafunio gani?

"Chochote kile mimi nakula."

"Nimekuuliza hivyo kwa sababu mimi nilinunua vitumbua ndivyo nilivyonyea chai, lakini vimebaki na kiporo cha wali na samaki jana, sasa labda wewe hutumii."

"Mmmh! We dada wewe, yaani mimi tena nianze kuchagua dunia yangu hii, wewe lete kilichopo mimi nakula," alisema huku akiwa ameshakaa kwenye kochi, sehemu ile ile ambavyo alikaa jana.

Zilipita kama dakika 10 hivi, geti likafunguliwa ikishiria kuna mtu anaingia na ni mwenyeji. Akaja mmoja kwa moja hadi kwenye mlango wa kuingilia sebuleni. Macho ya wote wawili walitazamana.

Kila mmoja akamshangaa mwenzake. Carry akashangaa zaidi kumkuta James nyumbani kwao kwa mara ya kwanza.

Hakumsemesha, akapilitiza moja kwa moja chumbani.

"Huyu amekuja kufanya nini hapa?" Lilikuwa ni swali la kwanza bila kumsalimia mdogo wake.

"Nimemwita mimi." Akajibu kwa kifupi na kwa sauti kavu.

"Kufanya nini we Catty, mbona mpana hivi kama boti la sinema?"

Ilibidi Catty amweleze kila kitu kilichotokea. Kutoka kumkuta chini ya mti jana, ugonjwa wake mpaka kumpa pesa ya kujitibia na kumwambia awe anakuja kula chakula hapo mpaka pale atakapojisikia vizuri, kupata nguvu na kuanza kufanya kazi zake kama zamani.

"Mdogo wangu utakuja kukaribisha vibaka hapa."

"We dada acha hizo, James tangu lini anakuwa kibaka, watu wote wa Kinondoni Moscow wanamfahamu, anafanya kazi mbalimbali na wakati mwingine za ndani ya nyumba yao sijawahi kusikia ameiba?" Akajibu Catty kwa hasira iliyomfanya dada yake atulie kidogo na kushusha pumzi.

"Au umemuelewa mdogo wangu, kama umemuelewa si useme tu!" Carry akasema huku akitabasamu.

Bado mdogo wake alimuangalia kwa hasira kidogo, halafu akamalizia kusema.

"Dada huyu naye pia ni binadamu, hebu angalia hana maisha mazuri, na tumefundishwa kwenye vitabu vitakatifu vyote kuwa tuwasaidie wahitaji, mtu kama huyu ukimsaidia na kumfariji akajiona ana thamani mbele za watu na wewe unabarikiwa na Mungu, hata milango yako ya riziki inafunguka. Unasemaje unampenda Mungu wakati bindamu mwenzako aliyeumbwa naye kama wewe unamchukia?"

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# HARMONIZE AING'ANG'ANIA WASAFI

MWANAMUZIKI Harmonize amefichua kwamba kuanzishwa kwa vituo vya redio na runinga ya Wasafi lilikuwa ni wazo lake.

Harmonize amesema wazo hilo alimshirikisha Diamond Platnumz na wote wawili walikuwa wakipanga na kununua vifaa vingi lakini baadae alipotoka aliviacha vyote na wala hakubeba hata kimoja.

"Wazo la kwanza lilikuwa ni chaneli ya mitandaoni na hilo lilikuwa wazo letu pamoja. Kufikia muda mimi nilisafiri kwenda Italia nilikuwa nimenunua vifaa ikiwemo na mashine za DJ na mashine nyingine nyingi, na tulipoanza tukasema kwa nini tusitafute mtu tukafanya naye kwa pamoja.. singependa kumtaja mtu huyo.. lakini vifaa vilikuwepo kwa sababu nilikuwa nimenunua mimi," amesema.





## 'NILITAKA KIJIUA'

MSANII mkongwe wa Nollywood, Chinedu Ikedieze, maarufu kama Aki, ametoboa siri kuwa alitaka kujiua baada ya kusikia ana tatizo la udumavu.

Muigizaji huyo amesema alichukua hatua hiyo baada ya kupata hofu baada ya kumsikia daktari akimwambia mama yake kuhusu hali yake.

Amesema alifikiria kukatisha maisha yake kutokana na matukio ya kuonewa na watoto wengine kwa sababu ya udogo wake wa kiumbo.

Alifichua kwamba katika mahojiano na mwanahabari maarufu nchini Nigeria, Chude Jideonwo.

Kulingana na Ikedieze dalili ya kutorefuka ilitokea alipokuwa na umri wa miaka tisa na miezi sita. "Nakumbuka daktari alimwambia mama yangu mwanao ana tatizo la ukuaji." amesema

"Hapo ndipo nilianza kusikia maneno, kudumaa na kuchelewesha ukuaji. Nililia mara kadhaa kwa sababu nilionewa shuleni na hata nyumbani kwa sababu sikukua kama wengine," ameongeza

Ameeleza alikuwa na hali mbaya, lakini alimshukuru Mungu kwamba alimpatia ujasiri wa kukubali hali yake.

Alisema anamshukuru mama yake kwa kusimama naye katika nyakati zote ngumu.

Ikedieze aliongeza kwamba tangu mara ya kwanza alipokutana na Osita Iheme, maarufu kama Pawpaw, hapo ndipo walipounda urafiki na kuigiza naye.

## ZISIKUPITE

### BALOGUN AWANIWA
CHELSEA wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Marekani, Folarin Balogun kutoka Arsenal, ambaye thamani yake ni pauni milioni 50, huku Monaco pia wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 na Inter Milan wakijitoa kwenye kinyang'anyiro cha kumsaka**. ( Sky Sports)**

### FRESNEDA AWINDWA
CHELSEA inataka kumnunua beki wa kulia wa Real Valladolid na Hispania, Ivan Fresneda lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 anataka kuhamia Barcelona. **(Mail)**

### SILVA ATASAINI
KLABU ya Manchester City ina imani winga wa Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 29, atasaini mkataba mpya licha ya uvumi kuhusu mustakabali wake msimu huu**. (90 min)**

### PETROVIC ATAKIWA
CHELSEA pia wanakaribia kutoa kitita cha pauni milioni 11.8 kwa mlinda mlango wa Serbia na New England Revolution, Djordje Petrovic mwenye umri wa miaka 23. **(Evening Standard)**

### AMRABAT BADO
KLABU ya Fiorentina bado haijapokea ofa rasmi kutoka kwa Manchester United kwa kiungo wa kati wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 26. **(Mirror)**

### CANCELO ATAKIWA BARCA
BARCELONA wapo kwenye mazungumzo ya kiwango cha juu na Manchester City ili kumsajili beki wa Ureno, Joao Cancelo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 anataka kuhama. **(Fabrizio Romano)**

### TANGANGA AWANIWA
KLABU ya Luton imetuma ya maombi ya kutaka kujua kuhusu mkopo kwa mlinzi wa Tottenham Hotspur, Japhet Tanganga mwenye umri wa miaka 24 **(Athletic)**

### VARANE ANASAKWA
MLINZI wa Manchester United na Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30, anasakwa na klabu ya Saudi Arabia Al-Ittihad. **(Express)**

### PSG YAMTAKA FATI
MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 20 amepewa ofa ya kwenda Paris St-Germain baada ya hapo awali kuhusishwa na Manchester United na Arsenal. **(Sun)**

### PAVARD AVUTIA
BENJAMINI Pavard wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 27 anabakia kuwa mmoja wapo wa wachezaji wanaolengwa na Inter Milan huku beki huyo wa Ufaransa akiivutia pia Arsenal. **(Evening Standard)**

### LINGARD HATAKIWI
KOCHA wa West Ham, David Moyes amedai kuwa kwa sasa hafikirii kumnunua kiungo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 30, Jesse Lingard. **(Mail)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AJA JUU KUHUSU FATI

**Ni baada ya kuulizwa kama kuna uwezekano wa nyota huyo kujiunga na mahasimu wao Real Madrid, asema ni...**

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez aliulizwa ikiwa ripoti zinazodai Ansu Fati anaweza kujiunga na Real Madrid zilikuwa za mzaha baada ya Carlo Ancelotti kusema wana mpango wa kumsajili fowadi huyo.

Fati mwenye umri wa miaka 20 amekuwa akiingia na kutoka katika kikosi cha kwanza cha Barca tangu apone majeraha kadhaa msimu uliopita wa joto na amekuwa akihusishwa mara kwa mara na kutaka kuihama klabu hiyo.

Wiki hii, kumekuwa na mazungumzo ya kuhama katika mgawanyiko wa Clasico, lakini Xavi anasema bado ana jukumu kubwa la kuichezea Barca.

"Huo ni utani au?" bosi huyo wa Barca alisema katika mkutano na waandishi wa habari Ijumaa alipoulizwa kuhusu Ancelotti kutoa uvumi wa kumsajili.

"Nilikuwa wazi sana kuhusu Ansu wiki iliyopita. Yeye ni rasilimali kubwa kwa klabu sasa na siku zijazo. Siwezi kuwa wazi zaidi.

"Sielewi mjadala unaozushwa karibu naye. Ni mchezaji wa Barca na tunamtegemea. Yuko katika hali nzuri na tunafurahishwa na uchezaji wake. Tunatumaini tunaweza kuacha kuzungumza juu ya hili kwa sasa kwa sababu haina maana."

Kocha wa Madrid Ancelotti hapo awali alisema: "Ninachoweza kusema ni kwamba Ansu Fati ni mchezaji mdogo mwenye vipaji vingi na atakuwa na mustakabali mzuri, nitaishia hapo."

Fati alifunga mabao 10 katika mechi 51 msimu uliopita, ingawa alitumika zaidi akitokea benchi. Pia aliingia kama mchezaji wa akiba katika sare ya bila kufungana ya Barca ya ufunguzi wa msimu dhidi ya Getafe wikendi iliyopita.

Baada ya kutokea eneo la tukio akiwa na umri wa miaka 16, mfululizo wa majeraha mabaya yamezuia maendeleo yake, na kusababisha Barca kufikiria kama uhamisho, ama kwa mkopo au wa kudumu, unaweza kuwa bora kwake.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
WEST HAM
VERSUS
CHELSEA
1 | 3.77
X | 3.48
2 | 2.01

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MAN CITY KUSAKA MBADALA DE BRUYNE

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City itaingia kwenye soko la usajili kutafuta mrithi wa Kevin De Bruyne, kwa mujibu wa Pep Guardiola.

Kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji ameondolewa kwenye klabu hadi mwaka mpya baada ya kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha jeraha la misuli ya paja.

City wametumia zaidi ya pauni milioni 100 kuwanunua Mateo Kovacic na Josko Gvardiol msimu huu wa joto lakini Guardiola amesema kuwa nje kwa muda mrefu kwa De Bruyne kunamaanisha wachezaji wapya zaidi wanahitajika.

"Tunazungumza sana na mkurugenzi wa soka, Txiki Begiristain kuhusu kile tunachopaswa kufanya, labda tunahitaji kuongeza mtu mwingine," alisema Guardiola.

"Maoni yangu ni napenda kikosi kidogo. Lakini pigo kutoka kwa Kevin kunabadilisha mtazamo.

"Ni mchezaji muhimu sana na sio wiki moja au mbili. Ni miezi minne au mitano. Kwa hivyo tunapaswa kutafakari kidogo juu ya kikosi, na kufikiria kile tunachopaswa kufanya."

Pamoja na kiungo mpya, City pia wanatafuta winga mwingine kuchukua nafasi ya Riyad Mahrez, ambaye alijiunga na Al Ahli kwa ada ya pauni milioni 30.

Mshambuliaji wa Rennes, Jérémy Doku ni chaguo moja lakini Guardiola amesisitiza kuwa City haitalipa fedha nyingi kwa mchezaji huyo.

"Lazima tuone nini kitatokea sokoni na kama tunaweza kufanya hivyo na kulipa kile tunachoamini ni haki," alisema Guardiola.

# Spalletti kocha mpya Italia

**ROME, Italia**

LUCIANO Spalletti atakuwa kocha mkuu mpya wa timu ya taifa ya soka ya Italia, Shirikisho la soka la nchi hiyo limetangaza, akichukua nafasi ya Roberto Mancini aliyejiuzulu Agosti 13.

Spalletti mwenye umri wa miaka 64 aliiongoza Napoli msimu uliopita kutwaa taji lake la kwanza la Serie A baada ya miaka 33, na kutwaa taji la uongozi wa klabu kwa muda mrefu ambao umejumuisha muda wa kukaa AS Roma, Inter Milan, na miaka mitano akiwa na klabu ya Zenit St Petersburg ya Urusi.

Aliachana na Napoli Mei baada ya kuomba likizo na nafasi yake kuchukuliwa na Mfaransa Rudi Garcia.

Shirikisho la Soka la Italia lilisema kwenye tovuti yake kwamba Spalletti atachukua wadhifa huo kuanzia Septemba 1.

"Timu ya taifa ilihitaji kocha mkuu na nina furaha sana kwamba alikubali,"



rais wa shirikisho, Gabriele Gravina alisema.

"Shauku yake na utaalamu wake utakuwa msingi kwa changamoto zinazoingoja Italia katika miezi ijayo."

Chanzo kimoja kiliiambia Reuters kwamba mkataba wa Spalletti utaendelea hadi Kombe la Dunia la 2026. Taarifa rasmi haikutaja urefu wa mkataba wake.

Spalletti atakuwa kocha wa tisa wa timu ya taifa katika karne hii.

Mechi yake ya kwanza akiwa kocha mkuu itakuwa ni ya kufuzu Euro 2024 huko Macedonia Kaskazini mnamo Septemba 9, na Azzurri watakuwa wenyeji wa Ukraine siku tatu baadaye.

Italia kwa sasa wako nafasi ya tatu katika Kundi C kwa pointi tatu katika mechi mbili, wakiwa nyuma ya Ukraine kwa pointi sita kutokana na michezo mitatu. England inaongoza kundi hilo ikiwa na pointi 12 baada ya mechi nne.

Wakati akiondoka Napoli, Spalletti alisema anachukua mwaka wa mapumziko na kuongeza kuwa anaweza kuwa wazi kufundisha timu ya taifa baada ya mwaka wake wa mapumziko.

CHEZA USHINDE KASINO

# KOCHA AZAM: HATUNA SABABU KUTOFANYA VIZURI LEO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema kwa namna alivyokiandaa kikosi chake na utayari wa wachezaji hana sababu ya kutopata matokeo mazuri katika mchezo wa leo wa Kombe la shirikisho Afrika dhidi ya Bahir Dar Kenema ya Ethiopia.

Azam leo ikiwa ugenini itacheza mchezo wake wa kwanza hatua ya awali ya michuano hiyo na ya pili kwa ukubwa kwenye ngazi ya vilabu Barani Afrika kwenye uwanja wa Abebe Bikila nchini humo.

Dabo alisema amekiandaa vizuri kikosi chake na ana matumaini ya kufanya vizuri ingawa mpira una matokeo matatu.

"Tumejiandaa vizuri, Vijana wamechangamka na wanautaka huu mchezo, tunafahamu tunacheza ugenini na wapinzani wetu pia watataka ushindi, lakini nakiamini kikosi changu na tumejiandaa, hatuna sababu ya kwa nini tusifanye vizuri ingawa matokeo ya mpira muda mwingine yanashangaza," alisema Dabo.

Alisema wanataka kumaliza mchezo leo ili wasiwe na kazi kubwa kwenye mchezo wa marudiano utakaochezwa Agosti 25 kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Azam Complex.

Kwa upande wake, Afisa habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, alisema kikosi chao kilifika salama nchini humo na bahati nzuri wamekuta hali ya hewa ya kawaida.

"Hali ya hewa haijawa changamoto kubwa kama ambavyo tulikuwa tukidhani wakati tunatoka Dar es Salaam, mchezaji pekee ambaye hatujasafiri naye ni Edward Manyama kutokana na majeraha madogo na kuumwa malaria, tuwaambie tu Watanzania kuwa tupo tayari kwa ajili ya mechi hii ya awali mkondo wa kwanza, kazi iliyotuleta huku ni kuipambania na kuipeperusha bendera ya Tanzania," alisema Ibwe.

Mara ya mwisho Azam kucheza michuano hiyo ilikuwa Oktoba 16 mwaka jana dhidi ya Al Akhdar ya Algeria kwenye Uwanja wa Azam Complex, Azam ikashinda mabao 2-0 lakini ilitolewa kutokana na kufungwa mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Oktoba 6 Algeria.

Mshindi wa jumla katika mechi mbili anatarajia kucheza na Club Africain ya Tunisia ambayo msimu uliopita ilitolewa na Yanga kwa kuchapwa bao 1-0 kwenye hatua ya mchujo kusaka timu zilizoingia hatua ya makundi ya kombe hilo.



Familia ya marehemu Peter Mwenda wakiwa na huzuni ndani ya Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam wakati wa kuuaga mwili wa mpendwa wao, Peter Mwenda kabla ya mazishi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga kusaka rekodi

INATOKA UK. 24

kwa tahadhari ili kupata matokeo mazuri.

Alisema ameiangalia Yanga kwenye baadhi ya michezo ukiwemo wa fainali ya kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita na kuona ubora wao.

"Hali ya hewa ya hapa Dar es Salaam ni tofauti na Djibouti lakini haitatuzuia kupambana na Yanga kwa sababu tumekuwa hapa kwa siku nne na kuzoea hali ya hewa, tutapambana kupata matokeo chanya katika mchezo ," alisema Kocha huyo msaidizi.

Baada ya mchezo wa leo utakaoanza saa 11:00 jioni, timu hzo zitarudiana Agosti 27 ili kumpata mshindi wa jumla atakayesonga mbele hatua ya kwanza ya michuano hiyo ambap[o mshindi atacheza na kati ya El Merreikh ya Sudan au AS Otoho ya Congo.

## Robertinho asisitiza

INATOKA UK. 24

Liyogope alisema wamejiandaa vizuri kutafuta matokeo chanya na wameona namna gani Simba wanacheza.

Alisema wanafahamu wanaenda kukutana na timu kubwa yenye wachezaji wazoefu lakini watapambana kuhakikisha wanafanikiwa kufanya vizuri na kusitisha uteja kutoka kwa wapinzani wao hao.

"Tumekuja kivingine kabisa hatutaingia kama tulivyocheza na Coastal Union, Simba wasitarajie kupata mchezo rahisi kwa sababu wachezaji na benchi la ufundi tunautaka huu mchezo," alisema Liyogope.

Katika mchezo wa leo timu zote zina kiu ya kupata matokeo mazuri na mchezo unatabiriwa utakuwa wenye upinzani mkubwa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 20/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4249 | Spain W vs England W | 2.60 | 2.85 | 2.75 |
| 14:00 | 1385 | Lille vs Nantes | 1.62 | 3.95 | 5.54 |
| 14:30 | 2183 | Anderlecht vs KVC Westerlo | 1.80 | 3.69 | 3.89 |
| 15:30 | 2390 | Sparta Rotterdam vs Feyenoord | 5.15 | 4.16 | 1.53 |
| 15:30 | 3451 | Twente vs PEC Zwolle | 1.32 | 4.95 | 7.73 |
| 16:00 | 2721 | Le Havre vs Brest | 2.78 | 3.24 | 2.62 |
| 16:00 | 3505 | Lorient vs Nice | 3.19 | 3.45 | 2.24 |
| 16:00 | 4857 | Aston Villa vs Everton | 1.70 | 3.90 | 4.83 |
| 16:00 | 5723 | Reims vs Clermont Foot | 1.84 | 3.80 | 4.11 |
| 16:30 | 2042 | Union Berlin vs Mainz | 2.02 | 3.39 | 3.86 |
| 17:00 | 2313 | Kilmarnock vs Celtic | 6.50 | 4.98 | 1.34 |
| 17:00 | 3464 | Chernomorets Odessa vs Dynamo Kiev | 5.63 | 4.13 | 1.45 |
| 17:00 | 3780 | KAA Gent vs St Truiden | 1.43 | 4.37 | 6.36 |
| 17:45 | 5193 | Waalwick vs AZ Alkmaar | 4.87 | 3.97 | 1.58 |
| 18:00 | 3562 | TSV Hartberg vs RB Salzburg | 8.86 | 4.53 | 1.29 |
| 18:05 | 5923 | Monaco vs Strasbourg | 1.79 | 3.82 | 4.33 |
| 18:30 | 1699 | Eintracht Frankfurt vs SV Darmstadt | 1.41 | 4.92 | 7.39 |
| 18:30 | 2631 | West Ham vs Chelsea | 3.77 | 3.48 | 2.01 |
| 19:00 | 2186 | Derry City vs St Patricks | 2.02 | 3.25 | 3.35 |
| 19:00 | 3222 | FC Kryvbas Kriviy Rih vs Shakhtar Donetsk | 5.66 | 4.14 | 1.45 |
| 19:00 | 4548 | Midtjylland vs Brondby | 2.23 | 3.27 | 3.12 |
| 19:00 | 5795 | Slavia Prague vs Banik Ostrava | 1.23 | 6.00 | 9.93 |
| 19:15 | 5967 | Basaksehir vs Fatih Karagumruk | 1.66 | 3.87 | 4.44 |
| 19:30 | 1003 | Sassuolo vs Atalanta | 3.45 | 3.55 | 2.09 |
| 19:30 | 1352 | Roma vs Salernitana | 1.60 | 3.84 | 6.02 |
| 19:30 | 5147 | Spartak Moscow vs Zenit St Petersburg | 2.37 | 3.39 | 2.67 |
| 19:50 | 3977 | Rudes Zagreb vs Hajduk Split | 7.29 | 4.45 | 1.34 |
| 20:00 | 2788 | Porto vs Sporting Farense | 1.12 | 7.36 | 16.90 |
| 20:00 | 3739 | Akhmat Grozny vs Gazovik Orenburg | 1.83 | 3.65 | 3.70 |
| 20:00 | 5067 | Girona vs Getafe | 2.06 | 3.13 | 4.06 |
| 20:00 | 5889 | PAOK vs Asteras Tripolis | 1.30 | 4.70 | 10.44 |
| 20:15 | 3694 | Stromsgodset vs Lillestrom | 3.10 | 3.52 | 2.09 |
| 20:15 | 5961 | Kortrijk vs Eupen | 2.11 | 3.69 | 2.94 |
| 20:30 | 2856 | Barcelona vs Cadiz CF | 1.27 | 5.72 | 11.08 |
| 20:30 | 3804 | Javor Ivanjica vs Backa Topola | 4.75 | 3.84 | 1.57 |
| 20:30 | 5194 | FK Napredak vs Mladost Lucani | 1.66 | 3.59 | 4.35 |
| 21:00 | 4887 | Odense vs Aarhus | 2.67 | 3.28 | 2.52 |
| 21:00 | 5908 | Legia Warszawa vs Korona Kielce | 1.41 | 4.34 | 5.85 |
| 21:15 | 1046 | Domzale vs NK Celje | 2.69 | 3.20 | 2.35 |
| 21:45 | 1783 | Lecce vs Lazio | 3.75 | 3.34 | 2.07 |
| 21:45 | 2329 | Udinese vs Juventus | 4.22 | 3.50 | 1.90 |
| 21:45 | 2524 | Besiktas vs Pendikspor | 1.30 | 5.11 | 8.31 |
| 21:45 | 3688 | Gaziantep BB vs Sivasspor | 2.53 | 3.46 | 2.49 |
| 21:45 | 3716 | Lens vs Rennes | 2.09 | 3.66 | 3.35 |
| 22:00 | 4151 | Bahia BA vs Bragantino SP | 2.74 | 3.18 | 2.38 |
| 22:00 | 4650 | Santos vs Gremio | 2.70 | 3.14 | 2.43 |
| 22:00 | 5297 | NK Osijek vs HNK Gorica | 1.70 | 3.68 | 3.98 |
| 22:00 | 5499 | Colo Colo vs Universidad Catolica | 1.65 | 3.55 | 4.67 |
| 22:05 | 4935 | HNK Rijeka vs Lokomotiva Zagreb | 1.59 | 3.83 | 4.53 |
| 22:30 | 2852 | Betis vs Atletico Madrid | 3.69 | 3.28 | 2.11 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumapili Agosti 20, 2023

Nipashe



## Xavi aja juu kuhusu Fati

UKURASA 21



Mshambuliaji wa Al Nassr ya Saudi Arabia, Cristian Ronaldo akimtoka beki wa Al Taawoun FC Hassan Kadesh kwenye mchezo wa Ligi kuu ya nchini humo juzi usiku, timu ya Ronaldo ilifungwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA KUANZA KUSAKA REKODI MPYA AFRIKA LEO

## Gamondi afichua mechi ya Ngao ya Jamii 'ilimuamsha', licha ya kutowafahamu wapinzani wao ajivunia...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga leo kinaanza safari ya kusaka rekodi mpya ya mafanikio kwenye michuano ya kimataifa itakapoikaribisha klabu ya AS Al Sabieh 'ASAS FC' kwenye mchezo wa kwanza hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku Kocha Miguel Gamondi akiweka wazi kuwa mchezo uliopita wa Ngao ya Jamii dhidi ya Simba ulimuamsha na kumpa kitu cha kufanyia marekebisho kabla ya mchezo wa leo.

Msimu uliopita Yanga iliweka rekodi yake mpya kwenye mashindano ya CAF kwa kucheza mchezo wa fainali ya michuano ya kombe la Shirikisho Afrika na sasa wanasaka rekodi mpya kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Gamondi alisema mafanikio msimu uliopita yanawapa chachu yakufanya vizuri zaidi kwenye michuano hiyo mikubwa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema kikosi chake kipo tayari kwa mchezo huo hasa baada ya kufanyia kazi mapungufu aliyoyaona wakati wakicheza michezo ya Ngao ya Jamii wiki iliyopita.

"Kwenye mchezo dhidi ya Simba wa fainali Ngao ya jamii yapo mapungufu kwa upande wa timu yangu niliyaona, nimeyafanyia kazi na naamini kwenye mchezo wa kesho (leo) sitoyaona na tutapata ushindi mzuri," alisema Gamondi.

Alisema kuwa wamedhamiria kufanya vizuri katika mchezo huo kwa kusaka ushindi wa idadi kubwa ya magoli ili mchezo wa marudiano wasiwe na wakati mgumu na kuweza kupata nafasi ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya Afrika.

Kikosi cha Yanga kinashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya msimu uliopita kumaliza mshindi wa pili wa Kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC), nyuma ya mabingwa USM Alger ya Algeria na kukosa taji hilo kwa kanuni ya bao la ugenini, ambapo walifungwa mabao 2-1 hapa nyumbani na wakashinda 1-0 ugenini.

Yanga iliangukia katika Kombe la Shirikisho baada ya kutolewa katika Ligi ya Mabingwa Afrika kufuatia kipigo cha jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

"Kusema kweli sifahamu hii timu (ASAS FC), msimu uliopita Yanga ilifanya vizuri kwenye mashindano ya Kimataifa, tunataka kufanya vizuri zaidi ya hapo, tumejiandaa kukabiliana na wapinzani wetu kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, tunataka kuendeleza furaha ya mashabiki wa timu yetu," alisema Gamondi.

Akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, beki wa pembeni wa timu hiyo, Nickson Kibabage alisema mchezo utakuwa mzuri na kuahidi kuwafurahisha mashabiki wao baada ya kupoteza fainali ya Ngao ya Jamii na Simba.

"Kocha Gamondi amefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwenye mechi iliyopita na wachezaji tunaotaka mcheo huu, tutahakikisha tunafanya vizuri dhidi ya Asas FC, hatutawadharau wapinzani wetu kwa kuona ni timu dhaifu, tutacheza kwa kuwaheshimu kwa sababu tunahitaji kusonga mbele na kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema Kibabage.

Aidha, Kocha Msaidizi wa ASAS FC, Mohammed Kader Daher alisema anafahamu Yanga ni timu kubwa kulinganisha na wao lakini wamejiandaa vizuri kukabiliana nao, watawaheshimu na kucheza

INAENDELEA UK 23

# Robertinho asisitiza pira 'biriani' wakisaka alama tatu nyingine leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo ikicheza mchezo wake wa pili wa ligi kuu kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam dhidi ya Dodoma Jiji FC, Kocha wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema bado timu yake haijaanza kucheza soka la kuvutia 'pira biriani' lakini amewahakikishia mashabiki ushindi leo.

Robertinho alisema taratibu timu yake inaanza kurejea kwenye utamaduni wake wa kucheza soka la kuvutia na muda si mrefu mashabiki watalifurahia.

Alisema wataingia uwanjani leo kwa lengo moja tu la ushindi ili kuendelea kuwa kwenye mbio za kufikia malengo yao msimu huu ya kutwa mataji yote ya ndani.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri yenye alama tatu, timu yangu ipo tayari kucheza kesho (leo), tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa ajili ya kutafuta ushindi ambao utaendelea kutupa hamasa ya kufikia malengo yetu msimu huu," alisema Robertinho na kuongeza,

"Bado hatujafikia aina yetu ya uchezaji, lakini taratibu tutafikia huko, unajua tunawachezaji wengi ambao wameingia kwa mara ya kwanza kwenye timu, lakini baada ya muda mfupi mashabiki wataendelea kufurahia soka safi, Simba ina aina ya kosa lake la kuvutia," alisema.

Robertinho alisema kwenye mchezo wa leo bado ataendelea kuwakosa wachezaji wake, Henock Inonga anayeuguza jeraha la bega na Aubin Kramo ambaye aliumia goti kwenye mazoezi ya timu hiyo.

Simba walianza vizuri msimu huu wa 2023/24 kwa kupata alama tatu ugenini mbele ya wenyeji wao Mtibwa Sugar na leo wanakibarua kingine cha mchezo wa Ligi Kuu utakaoanza saa 10:00 jioni.

Kwa upande wao Dodoma jiji FC ambao nao mchezo wao wa kwanza walipata ushindi wa mabao 2-1 mbele ya Coastal Union, kupitia kwa kocha wao Msaidizi Kassim

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002